Lile Juma La Sabini La Danieli

Asante, sana, Ndugu Neville. Habari za asubuhi, wapendwa. Ni majaliwa kuwa hapa tena katika maskani asubuhi ya leo, kuendeleza Ujumbe huu mkuu tunaojitahidi kuelezea, hili *Juma La Sabini La Danieli*. Nasi tuna furaha kuona wengi sana waliokusanyika hapa katika siku hii yenye joto, na hata hivyo tunasikitika ya kwamba hatuna nafasi ya kutosha ya kuketi. Kuona watu waliosongamana namna hiyo na wakisimama kila mahali, linakuwa si jambo zuri. Na kwamba hamjaketi kwa raha jinsi ambavyo mngepaswa kuketi, hilo linalifanya vigumu kwenu kuupata. Lakini tutafanya yote tuwezayo kuharakisha.

2 Na—na, leo, ninatumaini ya kwamba mtapata, kama nikichelewa kidogo, hilo mtanisamehe, kwa sababu huu ndio wakati wa kupiga nyundo Ujumbe huu, ni wakati halisi wa kuutilia mkazo. Tuliuweka katika sehemu tatu ili kwamba tuwe na uhakika wa kuupata.

3 Sasa, bila shaka, ku—kusanyiko lililopo hapa linajua ya kwamba hizi, ama Jumbe hizi, zinarekodiwa. Na zinatumwa kila mahali ulimwenguni. Karibu kila taifa linapokea kanda hizi ulimwenguni kote. Nami ningetaka kuwaambia wasikilizaji wa kanda jambo hili, po pote mlipo, katika sehemu yo yote ile ya ulimwengu mlipo, ya kwamba huenda kukawa na mambo fulani hapa ndani ambayo pengine msikubaliane nami juu ya mafundisho ambayo ni—ninafundisha. Lakini ningetaka kusema, ndugu, labda, kwamba kama ungalilielezea jambo hilo jinsi ulivyoliona, huenda likawa tofauti na vile ambavyo ningeamini mimi. Lakini, ningefurahi kusikiliza yale ambayo wewe ungesema.

4 Na ni kwa wazo hili ambapo ninazileta Jumbe hizi, kutoka. . .kwenye Neno la Mungu, moyoni mwangu. Ni kwa ajili ya kulijenga Kanisa, ni kwa ajili ya Kanisa lote, Kanisa la ulimwenguni mzima; Kanisa la Kristo, lililoko ulimwenguni kote. Nami kweli ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku ya mwisho. Na jitihada zangu za kuelezea jambo hili, na hata hivyo kutojaribu kulifanya ninii, kulishurutisha, kwa njia moja ama nyingine. Sijakuwa na hatia kamwe, nijuavyo mimi, ya kufanya jambo hilo.

5 Mara nyingi watu husikia kutoka kwenye kanda, na kusema, "Vema, sikukubaliana na jambo lile. Yeye hajui tu yale anayofundisha, hajui Maandiko." Vema, hilo, hilo linaweza kuwa ni kweli kabisa. Unaona? Nisingesema jambo hilo eti si kweli.

Lakini, kwangu mimi, ni—ninalisoma, bila kuchukua maneno yo—yote. . . Mimi husoma watu wengine wamesema

nini, na kuyathamini. Kila kitu anachosema mtu ye yote, ninakithamini. Lakini basi—basi ninalipeleka kwa Mungu, na kukaa nalo mpaka ninapoweza kulielezea, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, kisha ninaliona lote limeshikamana katika Biblia. Ndipo ni—ninajua liko karibu kuwa sawa. Na, bila shaka, pale ambapo wewe uko sahihi, hapo ndipo mahali pamoja tu nilipoondoka m—mstarini. Na labda mahali ulipokosea, ama ulipo sahihi, hapo ndipo mimi nilipokosea, na kadhalika.

6 Kwa hiyo, tunawathamini ninyi watu wote wazuri mliopo hapa mkutanoni, asubuhi ya leo, na ninyi watu wazuri mnaozikiliza kanda hizi. Nasi. . . Yote yanayofanyika, ni kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nina marafiki wengi wazuri sana kila mahali ulimwenguni, ambao ninawathamini sana, nami ninaamini ya kwamba nitaishi pamoja nao katika Umilele. Na lisingekuwa moyoni mwangu kujaribu—kujaribu kuwadanganya watu hao, kwa njia yo yote, lakini ni kujaribu kutimiza kila niwezacho kuwasidia.

7 Ninajisikia kama Sulemani alivyojisikia wakati alipoomba, na kusema, apewe hekima ili kwamba aweze kuwaongoza watu wa Mungu. Hilo ni ombi langu kutoka moyoni.

8 Wenzi wangu waliopo pamoja nami hapa, hapa, ninamwona Ndugu Mercier, na—na Ndugu Roy Borders, na Ndugu Neville, na Billy Paul, mwanangu. Gene yuko hapa mahali fulani, na hawa ndugu, Teddy, na hao wengine. Ninawathamini watu hawa wote wanaokuja kunisaidia.

9 Ninakumbuka hapa si muda mrefu uliopita, Ndugu Leo, o—ono alilokuwa nalo; ndoto, ndivyo alivyoiita, usiku mmoja tulipokutana mara ya kwanza; ya kwamba aliona kilele kikubwa cha piramidi, mbali huko juu kabisa hewani. Na mimi nilikuwa huko juu nikihubiri, mahali fulani, naye akapanda apate kuona ilikuwa ni kitu gani hasa. Na wakati alipofikia kule kwenye kilele hiki, mbona ninii, akasema, yaani mbali huko juu kabisa hapa namna fulani ya mwanga kama wa fedha, ama kama sahani, nilikuwa nimesimama, nikiwahubiria watu. Naye akaniashiria, ndipo nikageuka nikamwangalia. Basi akasema, "Ulipandaje ukafika huko? Ningewezaje kuja huko?"

10 Nikasema, "Leo, hakuna mtu awezaye kuja hapa. Mtu hana budi kuletwa na Mungu hapa. Sasa, hupaswi kuja huku juu. Unapaswa kushuka na kwenda kuwashuhudia hao watu kule chini, baada ya wewe kuona jambo hilo, ya kwamba ni Kweli, ya kwamba Jambo Hilo ni Kweli." Leo akashuka chini, kuwashuhudia watu.

11 Huo umekuwa ni muda gani, Ndugu Leo? Miaka mingi, sivyo? Miaka mingi. Tangu wakati huo, kadiri nijuavyo mimi, amekuwa mwaminifu katika kufanya jambo hilo, kuwashuhudia watu ya kwamba huduma hii inatoka kwa Mungu. Sasa, nami—nami sitaki itoke kwangu. Kama inatoka kwangu, basi haifai

kitu, kwa sababu hakuna jambo jema ndani ya mtu. Mnaona? Halina budi kutoka kwa Mungu.

12 Basi, ninapoangalia kila mahali . . . Jana alasiri, nilipeana mikono na rafiki yangu, Ndugu West. Sijamwona bado, humu jengoni; ndiyo, nimemwona sasa, asubuhi ya leo. Nanyi mnajua jinsi watu hao wanavyotoka mbali kwa gari, huko mbali kutoka—kutoka huko Alabama, Jumapili, wapate kufika hapa, kutoka huko mbali sana Alabama!

13 Ndugu Welch Evans, sikumwona Jumapili iliyopita. Kuna mtu fulani alisema alikuwa hapa leo. Watu hao husafiri kwa motokaa kutoka Tifton, Georgia, wapate kufika hapa. Pia ndugu anayeketi hapa, wenziwe. Wengi sana! Ndugu Palmer kutoka Macon, Georgia. Nami ninamwona, ninaamini, Dada Ungren na hao wengine kule nyuma. Wote wametoka huko mbali Memphis, Tennessee. Sasa, mnafikiri . . . Na wengine kutoka mahali mbalimbali. Nimekutana na mama mmoja sasa hivi hapa ndani kutoka, huko mbali Carolina ya Kusini.

14 Sasa, mnafikiri ya kwamba watu hapa . . . Nilikuwa nikiangalia huko, kutoka Chicago, na sehemu mbalimbali tu, wakiendesha magari yao mamia na mamia ya maili, ili kuhudhuria tu ibada. Halafu, wanapofika hapa, hakuna nafasi ya kuketi chini. Si chumba chenye kibaridishi; jengo la kale lenye joto, kusimama humo, wakifuta jasho. Wakichukua fedha kutoka mezani, kutoka kwa watoto wao, waje hapa kusikiliza Ujumbe huo. Unataka kuniambia hakuna . . . ng’ambo ya kijito hiki, mahali fulani, kwamba hakuna mahali wanapokwenda, moja ya siku hizi? Hakika, kupo. Huo ni uaminifu! Watu hao ni wenye kutoa zaka. Si kwamba wao wanakuja tu, wao wanaleta pia zaka na matoleo yao, na kuzileta katika nyumba ya Bwana, wakijaribu kufanya yaliyo sahihi. Mungu na awabariki sana watu waaminifu kama hao! Rehema za Mungu na neema ziambatane pamoja nao.

15 Ninamwona rafiki yangu, Charlie Cox, wale wanaotoka huko Kentucky ya kusini. Na ni kila mahali tu, ukiangalia kila mahali, unaona watu kutoka sehemu mbalimbali.

16 Huyu mwanamume kijana anayeketi pale, siwezi kukumbuka jina lake. Nilikutana naye huko Chicago. Lakini unatoka shule fulani ya Biblia mbali na mahali hapa, mahali fulani, sivyo? [Huyo ndugu anasema, “Springfield, Missouri”—Mh.] Springfield, Missouri; Shule ya Biblia ya Assemblies of God. Naam. Vema, vizuri. Unaona, wao wanatoka kila mahali tu, katika maskini kanisa hili dogo sana.

17 Hebu wazia tu, yapata, kama miaka thelathini iliyopita nilipoweka lile jiwe la pembeni asubuhi ile, nilikuwa nimesimama pale kwenye Barabara ya Saba, umbali wa jengo moja la mji. Sikuwa hata nimeoa bado, ni kijana mwanamume tu. Nami nikaona ono la watu wamesongamana

hapa ndani na kubanana kutoka kila mahali. Nami nilifurahi sana, nikiwa nimesimama nyuma ya mimbara. Na hapo ndipo Yeye aliponiambia, “Lakini hii si maskani yako.” Naye akaniketisha chini ya mbingu. Nanyi mnajua hadithi yote ambayo imeandikwa kwenye ukurasa wa kwanza wa Biblia uliowekwa kwenye jiwe la pembeni pale.

18 Ninawashukuru sana ninyi watu. Siwezi. . .Hilo, hilo ni dogo sana, ku—kusema tu, “Vema, ninawashukuru.” Lakini ninawaombea. Ninawaamini. Ninaamini katika matukio yenu na Mungu. Siamini ya kwamba mwanamume ama mwanamke angeendesha gari mamia na mamia ya maili kuja hapa, ili kuonyesha anavaa nguo za namna gani. Si—sidhani wangefanya jambo hilo. La. Hawangekuja hapa kusudi tu wapate kuonekana. Wao wanakuja hapa kwa sababu ni waaminifu tena sana kwa ajili ya wokovu wa nafsi zao. Ombi langu ni: “Mungu nisaidie, nisaidie niwe hata na nusu tu ya uaminifu huo, kujaribu kuwahudumia kwa yote yaliyo ndani ya moyo wangu, na kumtazamia Mungu.”

19 Ujumbe huu, mnaona, asubuhi ya leo, umechorwa hapa kwenye ubao hapa. Kwa namna fulani ni kwa ajili ya kufanya tu ninii, kuelezea ninapoendelea, kujaribu kufanya hivyo ili kwamba mpate kuelewa yale ninayojaribu kusema.

20 Na haya *Majuma Sabini Ya Danieli* yamekuwa ni somo moja kubwa, siku mbili mchana na usiku, karibu, nimekuwa, mwishoni mwa juma hapa, nimekuwa nikiendelea nazo, nikijaribu kupata maneno ya kusema kwa ajili ya Kweli. Hayana budi kulingana na Biblia yote. Unaona? Huwezi kuyachukua tu, Andiko moja dogo tu na ku—kulielezea lieleweke, na halafu useme, “Vema, hivi ndivyo hili linavyosema,” kisha ugeuke na kusema, “Vema, lakini mahali hapa li—linasema jambo lingine, linapinga jambo *hili* hapa.” Haliwezi kufanya hilo. Halina budi kusema jambo lile lile wakati wote. Kama hufanyi hivyo, mbona, hilo, basi ume—umekosea. Na hivyo ndivyo jinsi nilivyojaribu kufundisaha Jambo Hilo.

21 Jambo lingine, kwenye kanda, kwa kuwa sasa yananaswa. Upinzani mkubwa sana nilio nao kwenye kanda, kutoka kwa ndugu zangu katika sehemu mbalimbali ulimwenguni, ni kuamini katika neema ya Mungu, ambapo ninafundisha jinsi vile ninavyofundisha, ya kwamba, “Tulichaguliwa tangu zamani kabla ya mwanzo wa ulimwengu.”

22 Ndugu zangu wa Kipentekoste, bila shaka, ninajua ya kwamba mawazo yenu ni ya washika sheria, mnaona, na ni—ninajua kidogo linatatiza maoni yenu. Lakini, wewe kama ndugu Mkristo, je! mbona usilitafakari vya kutosha na kupiga magoti mbele ya Mungu, ukiwa na Biblia yako, na umwombe Mungu akuelezee jambo hilo? Ungeweza kufanya jambo hilo?

Ungechukua msimamo wa kisheria na kujaribu kulifanya liungane kutoka Mwanzo hadi Ufunuo?

23 Na, "Uzao wa nyoka," hilo ndilo linaloua; watu wengi hawaamini hilo. Lakini, kama utasoma tu katika Mwanzo, Biblia ilisema ya kwamba nyoka alikuwa na uzao. "Nami nitaweka uadui kati ya uzao wa nyoka na Uzao wa mwanamke." Kwa hiyo, nyoka alikuwa na uzao. Na kama uzao wa nyoka ulikuwa ni wa kiroho, basi Yesu hakuwa mwanadamu, kwa hiyo Uzao wa mwanamke ulikuwa wa kiroho. Wote wawili walikuwa na uzao, na uadui ungali bado upo. Nyoka alikuwa na uzao. Na kama utaichukua tu Biblia yako, na upige magoti uwe mwenye uchaji sana mbele za Mungu, ninaamini Mungu atalifunua kwako.

24 Na kama huelewi na jambo hilo, mimi ni—ninapatikana, wakati wo wote, kufanya niwezavyo kukusaidia, kwa barua ama kwa—kwa mazungumzo ya kibinafsi, ama kwa cho chote kile ambacho ningeweza kufanya kukusaidia nacho. Bila shaka, tunatambua ya kwamba hilo halimwokoi mtu, wala halimhukumu mtu, lakini linaleta tu Mwangaza juu ya somo ambalo tunajaribu sana kuwafanya watu waone. Mnaona? Linaleta Mwangaza tu.

25 Sasa, kwa wasikilizaji wanaoonekana, nilisema jambo hili kwa ajili ya hizi kanda, mnaona, na kanda hizi zinaenda kote, kila mahali.

26 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, kabla hatujamkaribia Mwandishi wa Neno hili. Na ni wangapi katika mkutano huu asubuhi ya leo wana haja, kusema tu, "Mimi ni mhitaji. Ee Mungu, nirehemu mimi"? Bwana awabariki. Na kwa hao watakaosikiliza kanda hii, mtakapoisikia, Mungu na awajalie haja yenu.

27 Baba yetu uliye Mbinguni, sisi ni watu wenye shukrani, hata hivyo tu watu wasiostahili. Lakini tunakikaribia Kiti Chako cha neema asubuhi ya leo, kwa sababu kwamba tumealikwa kuja. Yesu alisema, "Mkimwomba Baba jambo lo lote katika Jina Langu, nitalifanya." Sasa, tunajua ya kwamba jambo hilo ni kweli.

28 Na hapa katika wasikilizaji, na huko nje katika—katika nchi ambako kanda hizi zitaenda, labda kutakuweko na makumi elfu mengi ya Wakristo waliozaliwa mara ya pili watakaosikia jambo hili. Nasi tunajua, Baba, ya kwamba tunapozaliwa mara ya pili, ya kwamba roho yetu inazaliwa kutoka Juu. Ni Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, juu yetu. Nasi tunatambua ya kwamba Roho Mtakatifu huyo ana nguvu zote na anaweza kutufanyia jambo lo lote tunalotamani atufanyie. Basi, Baba wa Mbinguni, tungekuomba uachilie imani yetu kwa Roho huyo, ili aweze kutupatia sisi asubuhi ya leo, na kwa ajili ya utukufu wa Ufalme wa Mungu, haja hizi zote na shauku, ili kwamba tuponywe

magonjwa na mateso yetu, tupate kumtumikia Mungu wetu kwa yote yaliyo ndani yetu.

29 Fungua maskio yetu ya ufahamu leo, na ninapojitahidi kuleta swali hili kuu, na kulitatua katika mawazo ya watu. Sasa, nimeliandika hapa, Bwana, kwenye karatasi, na pia kulichora kwenye ubao huu, jedwali hii, lakini mimi sitoshelezi kabisa kulielezea. Sasa tunakuita Wewe, Mwalimu mkuu uliyeliandika hili Neno, uliyelivuvia, uliyempa Hilo nabii Danieli. Nasi tunaomba ya kwamba utatupelekea upako asubuhi ya leo, katika siku hizi za mwisho, kwa kuwa Yeye alisema ya kwamba kile Kitabu kitafungwa mpaka wakati huu, ya kwamba utafungua ufahamu wetu. Na jalia kuwepo na imani nyororo moyoni mwetu ambayo italiacha Neno lishikilie na lipate Uzima, na kuzaa miti ya haki katika maisha yetu, ambayo liimekusudiwa kuleta. Imani yetu katika Mungu, na ituletee hilo asubuhi ya leo. Kwa kuwa tunakungojea kwa unyenyekevu sasa, na tunajiweka wakfu Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

30 Sasa tunashukuru kwa asubuhi ya leo, kwa ajili ya nafasi hii nzuri tena kufungua kurasa hizi za Neno la Mungu la Milele.

31 Sasa, sababu ya mimi kuchukua jukumu la kujaribu kuelezea jambo hili, ni kwa sababu tunapitia katika Kitabu cha Ufunuo, na ndiyo tu tumalizie nyakati saba za kanisa. Na, tena, katika mwisho wa sura ya 3 ya Kitabu cha Ufunuo, Kanisa linanyakuliwa kutoka duniani, kwenda Utukufuni. Nami nikijaribu, kwa moyo wangu wote, kuwaletea watu jambo hili, ya kwamba wao wanatarajia jambo fulani kutukia, ambalo wameona limeandikwa katika Kitabu cha Ufunuo, wakati halikuwa linatumiwa kwa wakati wa kanisa. Nasi tunakaribia wakati wa mwisho kuliko mnavyofikiria.

32 Siku chache ziliopita usiku, Billy, ninii wangu . . . Ama, mkaza mwanangu, hasa, alinipigia simu, usiku sana, akasema kulikuwa na mtu jina lake Andy Herman, ambaye ni binamu yangu, alikuwa amelala, akifa hospitalini. Nilitoka nikaenda kumwona. Walikuwa wamempa dawa ya kulevya kupita kiasi, mimi . . . nyingi sana, hata alikuwa amelala, nami sikuweza kuzungumza naye. Asubuhi yake . . . Nikamwomba Mungu amweke hai mpaka nitakapoweza. Andy ni mtu mzuri, lakini ni kwamba tu yeye hakuwa ni Mkristo. Yeye si mjomba; ni binamu, alimwoa binamu yangu.

Na halafu wakati Shangazi Ade aliponiambia, akisimama pale, alisema, “Billy, miaka yote hii themanini ya maisha yake, yeye hajamtumikia Mungu. Lakini,” kasema, “majuma machache yaliyopita alikuwa ameketi nyumbani . . . ” Yeye, umri wa miaka themanini, bila shaka, yeye hafanyi kazi nyingi za mikono. Lakini alisema . . .

Yeye alimwita na kusema, “Ade, unajua nini? Kristo alikuja mbele yangu hapa, dakika chache tu zilizopita.”

Akamwangalia, akasema, "Andy, wewe—wewe. . . Kuna nini?" Akasema. . .

Yeye akasema, "La. Yeye alisimama papa hapa mbele zangu, kisha akasema jambo fulani."

Kasema, "Alisema nini?"

"Siku zimeenda kuliko unavyodhania."

33 Katika majuma machache tangu wakati huo, majuma mawili ama matatu, alikuwa ameshikwa na stroko na alikuwa amelala hospitalini, anakufa. Nikasema, "Shangazi Ade, huna aibu kwa kukosa kuniita ama mtu fulani, ili niuweke moyo wake katika hali nzuri kwa ajili ya saa hii ambayo sasa ameifikia."

34 Nikamwomba Bwana, asubuhi yake, wakati nilipo-. . . Hakuweza kuongea, kwa hiyo nilimwuliza tu. Nikasema, "Unaweza kunisikia, Mjomba Andy?" Naye a—aliweza kutikisa kichwa chake kidogo na kufungua taya zake. Nikamwombea, nikamfanya atubu dhambi zake mbele za Mungu. Nilitaka kumbatiza, naye Aunt Ade alitaka kubatizwa.

35 Ndipo nikashuka nikaenda ukumbini, kumwona maskini mama mmoja kijana anayeishi karibu nasi hapa, ambaye walikuwa wanataka kumpeleka kwenye hospitali ya wenda wazimu, naye Bwana alimfanyia jambo kubwa, akaja nyumbani.

Ndipo, nilipokuwa nikipanda njiani, nikakutana na dada mweusi, naye akasema, "Wewe siye Ndugu Branham?"

Akasema, "Ni mimi."

Akasema, "Unanikumbuka? Mimi ni Bibi. Drye."

36 Nami nikasema, "Ndiyo, ninaamini ninakukumbuka. Pete Drye na hao wengine." Nikasema, "Ndiyo, ni—ninakukumbuka." Akaangalia chumbani, na wakati tuliponinii. . . nikashangaa kwa nini alisema jambo hilo. Na, hapo, Mjomba Andy alikuwa tayari ameamka kitandani, ameketi pale, akisogeza mikono na viungo vyake kama mtu mwingine ye yote yule, akijaribu kushika kile kitu, kile kitu chini ya kitanda, ili aweze kutoka pale na kuenda zake. Sasa wao wanakuja kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu, yeye na mke wake.

37 Kwa hiyo, lakini sababu ya mimi kulisema jambo hilo, ni kwamba wakati umeenda sana kuliko tunavyofikiria. Nami ninaamini ya kwamba haya *Majuma Sabini Ya Danieli* yatatufanya tufahamu.

38 Sasa, karibu ndugu zetu wote wa Kipentekoste, jambo ambalo nililisema mapema kwenye kanda, ya kwamba wao hawakubaliani na jambo Hili. Wanatazamia kitu kikuu, chenye nguvu kitukie. Na, ndugu zangu, kama mtasikiliza kwa makini kabisa, wala msininii. . . na msikilize, mtaona ya kwamba hilo jambo kubwa, lenye nguvu limepita tayari. Yesu yuko tayari kurudi.

39 Kanisa linaondoka kwenye sura ya 3 ya Ufunuo. Hakuna jambo limesemwa mle ndani juu ya cho chote kile, lakini jambo la mwisho lilikuwa tu ni yule mjumbe wa mwisho wa wakati huu. Halafu, tunashughulika na Wayahudi mpaka kule kuja tena na Bibi-arusi, katika sura ya 19. Kutoka sura ya 6 mpaka ya 19 zote ni Wayahudi.

Hayo ndiyo ninayotaka kumwambia ndugu yangu mwema hapa wakati wa hii Muhuri, Ndugu Woods, ambaye hapo awali alikuwa Shahidi wa Yehova, yeye na familia yake yote, hapa asubuhi ya leo, ya kwamba wale "mia na arobaini na nne elfu" hawakuwa, hawakuwa na uhusiano wo wote na Mataifa. Ni Wayahudi. Mnaona? Wala si ule Mwili wa siri wa Kristo duniani leo.

Bibi-arusi ndiye huo Mwili wa siri. Kwa Roho mtakatifu tumebatizwa katika Mwili huo wa siri.

40 Sasa, tunajua ya kwamba katika Kitabu cha Danieli hapa, ambapo tulikuwa tukisoma, tutakisoma tu tena kwa sababu ni Neno Lake. Katika sura ya 9 ya Danieli, aya ya 24.

> *Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu, ili kukomesha makosa, . . .kuishiliza dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu, na kuleta haki ya milele, na kutia muhuri maono na unabii, na kumtia mafuta yeye aliye Mtakatifu sana.*

Aya ya 25, "Basi ujue na kufahamu, ya kwamba tangu . . ." Sikiliza, hilo ndilo tulilokuwa tukizungumzia, na tulimalizia hilo Jumapili usiku, "kupatia mafuta palipo Patakatifu sana." Hapa ndipo tutakapoanzia asubuhi ya leo, kwenye aya ya 25. "Na kwa hiyo . . ."

> *Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengengeza na kuujenga upya Yerusalemu* (yaani "mji wako mtakatifu," unaona) *hata zamani za Masihi aliye Mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu.*
>
> *Na baada ya yale majuma sitini na mawili, masihi atakatiliwa mbali, lakini si kwa ajili yake; na watu wa Mkuu atakayekuja watauangamiza mji, na patakatifu; na mwisho wake utakuwa pamoja na gharika, na hata mwisho ule vita vitakuwako; ukiwa umekwisha kukusudiwa.*

"Na . . ." Sasa, kumbuka, huo ndio mwisho wa vile vita. Tunalo kwenye ubao hapa. "Na," sasa tunaanza jambo lingine.

> *Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo*

la uharibifu; na hivyo, *hata ukomo*, (hiyo ni kusema, yote) *na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu ya mwenye kuharibu.*

41 Loo, ni somo la namna gani! Nilimwambia mke wangu hivi majuzi, "Sijui kama kweli watu wanalipata." Sasa, ninawatakeni mlipate. Msi-. . . Kama ninyi, inatubidi kukaa hapa siku nzima, tukae tu. Sasa, sisi—sisi—sisi tunataka kulipata. Mnaona? Tu—tunataka kujua ya kwamba ni Kweli. Na, nyinyi, laiti mangaliweza tu kuliona! Nami nitawauliza, labda . . .

42 Halafu tena, baadaye, nitaiacha jedwali hii ining'inie hapa, na ninyi m—mnaweza kuichora, baadaye. Njoni hapa alasiri ya leo, wakati wo wote mnaotaka, na mchore jedwali hizi na kadhalika. Zitawasaidia kufahamu. Hiyo ndiyo sababu niliiweka pale, kusudi mpate kufahamu.

43 Sasa, hebu na turudie kidogo tupate kupata msingi. Sasa kulikuweko na . . . Danieli alikuwa anahusika juu ya watu wake, kwa sababu alikuwa amemsoma nabii Yeremia, na akafahamu ya kwamba Yeremia alikuwa amesema ya kwamba wangekuwa uhamishoni kwa muda wa miaka sabini. Halafu basi, alikuwa ameona basi walikuwa tayari wamekuwa uhamishoni kwa muda wa miaka sitini na minane, kwa hiyo yeye alijua wakati ulikuwa umekaribia. Kwa hiyo aliwekea kando kazi zake zote, akashusha, kama kawaida, mapazia ya kazi zake zote za kila siku. Akauelekeza uso wake kwa Mungu, akavaa magunia na majivu, akaanza kufunga na kuomba, apate kufahamu wakati huo utakuwa lini. Ndipo tunaona, kama nilivyosema hapo awali . . .

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani jukwaani—Mh.] Tafadhali geuza hilo, kuelekea upande *ule*, kidogo tu. Hicho kibaridishi, kimezidi tu kidogo. Kinanifanya kupwelewa na sauti. Halafu . . . Asante, ndugu.

44 Sasa, kwa vile tunaona ya kwamba, Danieli, alitaka kupata habari hizi kwa ajili ya watu wake. Nami nafikiria ninii, kama Danieli, kwa kusoma manabii waliomtangulia, naye alikuwa na ufahamu wa namna hii, ya kwamba alikuwa karibu na mwisho, na akamsihi Mungu kwa maombi, apate kujua ule mwisho ulivyokuwa karibu; basi ninafikiri tuna haki, kwa kuona ya kwamba tuko mwishoni mwa barabara sasa, kuvaa si nguo za magunia na majivu, lakini tutupilie mbali mambo ya ulimwengu, na masumbuko yetu ya maisha haya; na tumtafute Mungu, tupate kujua ni siku gani ya mwaka tunayoishi ndani yake, kwa sababu tunaona tuko katika mwisho, na ili kwamba Kanisa litafunga na kuomba na kuwa tayari. Hiyo ndiyo sababu nimejitahidi kuchukua jukumu juu yangu . . . Bila kujua jinsi ya kulielezea jambo hili, kwa sababu nimelipita kila wakati, na kusema, "Hayo majuma sabini ya Danieli," kwa sababu

sikuweza kuyafahamu. Na hiyo ndiyo sababu nimechukua jukumu juu yangu sasa, kujaribu kuyaelezea. Nami ninaamini, kwa msaada wa Bwana, ninaweza kufanya jambo hilo kwa neema Yake, kulifikisha mahali ambapo, kuwaonyesha jinsi tulivyo karibu na kule Kuja kwa Bwana.

45 Sasa, Danieli alikuwa tu katika miaka miwili. Halafu tunaona, ya kwamba, wakati alipokuwa katika maombi, Malaika, Gabrieli, alimwendea haraka; na si kwamba alimwelezea tu ni lini watu wake watatoka uhamishoni, lakini, pia, yote yaliyokusudiwa kwa ajili ya watu wake, yote yaliyokuwa yamesalia kwa ajili ya watu wake. Alisema, "Kuna majuma sabini bado yaliyosalia kwa ajili ya Wayahudi."

46 Halafu, tunaona, ya kwamba alikuwa na makusudi sita. Moja la hayo, lilikuwa ni kukomesha makosa; na—na kuishiliza dhambi; kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu; kuleta haki ya milele; kutia muhuri ono na unabii; na kumtia mafuta aliye Mtakatifu sana.

47 Nasi tumechukua, Jumapili iliyopita asubuhi, Danieli katika hali yake kule, akiomba. Jumapili iliyopita jioni, tukitoa Maandiko, ili kwamba watu wapate kuyasoma watakapofika nyumbani. Mliyasoma? Mliyapenda? Vizuri sana!

48 Sasa, zile sababu sita. Nasi tunaona ya kwamba, kwenye kusudi hili la sita, "kumtia mafuta aliye Mtakatifu sana," tunaona ya kwamba "aliye Mtakatifu sana" daima liliwakilisha Kanisa, ile Maskani. Na jambo la mwisho lililopaswa kufanywa, lilikuwa ni kutia mafuta mahali Patakatifu sana, hiyo ni ile Maskani ya ule Utawala wa Miaka Elfu ambamo Yeye ataishi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, ambamo tutaishi.

49 Sasa, leo, sasa tunakaribia, "Yale majuma sabini ni nini?" Na hii ni sehemu iliyo muhimu sana, yale majuma sabini.

50 Sasa, tunajua ya kwamba Maandiko hayawezi kusema uongo. Hayana budi kuwa ni Kweli. Na kama Malaika huyu Gabrieli alikuja na kumwambia Danieli ya kwamba kuna majuma sabini tu yaliyosalia kwa ajili ya Wayahudi . . . Sasa, tungewekea jambo hilo kwa siku sita . . . ama juma la siku saba. Lakini, katika unabii daima yanatolewa katika mifano.

51 Na kwa hiyo, hapana shaka ya kwamba katika nyakati zote zilizopita, kumekuweko na mamia mara mamia ya watu, wanachuoni, watu wenye uwezo, wakijaribu kuelezea haya majuma sabini yalikuwa ni nini. Nami nimesoma mengi ya maelezo yao juu ya jambo hilo. Nami ninashukuru sana kwa ajili ya Bw. Smith, wa kanisa la Sabato, kwa ajili ya maoni yake. Ninashukuru kwa ajili ya Dk. Larkin, kwa maoni yake. Ninashukuru kwa ajili ya hawa wanachuoni wote wakuu, kwa ajili ya maoni yao juu ya jambo hili. Na katika kuwasoma, linanipa mwangaza sana, ya kwamba ninaweza kupata mahali panapoonekana kwamba ni sahihi. Lakini kupata maoni ambayo

ni—nilifikiri ningeweza kueleza, nilitafuta sana kwenye kitabu cha maarifa yote, juu ya "wakati," kutafuta kujua maana ya "wakati."

52 Na tunaona hapa ya kwamba, tuna "wakati, wakati na nusu wakati." Wakati ni nini? Juma moja ni nini? Sasa, hiyo imekuwa ni miaka elfu tatu, mia nne na thelathini iliyopita, tangu jambo hili lilipokuwepo, tangu Mungu alipoanza kuwashughulikia Wayahudi; miaka mingi, mingi iliyopita. Danieli alikuwa K.K., na wakati huo ilikuwa ni 538 K.K., miaka 538 kabla ya Kristo, wakati aliponena jambo hili la "wakati, wakati, na nusu wakati." Na, majuma sabini, angalia ambapo majuma sabini yangemchukua. Mbona, yeye alikuwa angali huko Babeli, katika majuma sabini, na hata hivyo Mungu alimwambia ya kwamba huo ndio wakati wote uliokusudiwa juu ya watu wake.

53 Sasa, kanisa langu hapa linajua ya kwamba daima katika miaka yote nimewaambieni, "Mkitaka kujua ni siku gani ya juma, angalieni kalenda. Lakini mkitaka kujua wakati tunaoishi, waangalieni hao Wayahudi." Hicho ndicho kipimo tu cha wakati. Mungu ha—hakuweka nyakati fulani zo zote kwa ajili ya Mataifa; hakukuweko na kipindi fulani cha wakati. Na hapo ndipo ninapofikiri ya kwamba waandishi wengi mashuhuri walipochanganyikiwa, na walikuwa wakijaribu kuwekea haya kwa Myahudi na Mmataifa, kwa sababu alisema, "Watu wako." Lakini alikuwa akinena na Danieli, si na Kanisa; watu wa Danieli, Myahudi. Kama angalikuwa akizungumza na Kanisa, huwezi kulifanya jambo hilo lifikie mahali po pote; una—unarudi nyuma kabisa, hata kabla ya kule kuja kwa Kristo. Lingeishia katika namna yo yote ya majuma ya kinabii ungalitaka kuyaweka ndani yake. Tayari yameisha. Lakini Yeye alikuwa anawazungumzia Wayahudi, kwa hiyo basi Wayahudi ndio saa ya Mungu.

54 Mnakumbuka hapa, si muda mrefu uliopita, wakati Ndugu Arganbright, wa California, makamu wa rais wa Shirika la Kimataifa la Wafanya Biashara wa Injili Yote, alipokuja nyumbani kwangu na kuleta ka—kanda; na si kanda, bali si—sinema, ambayo wao. . .ya *Usiku Wa Manane Kasoro Dakika Tatu*. Hiyo ilichukuliwa katika utafiti wa kisayansi. Nilipowaona hao Wayahudi wakirudi, wakirudi Yerusalemu, nikaja hapa maskanini, na kusema, "Najisikia kama nimeongoka upya." Wengi wenu mnakumbuka jambo hilo. Nilisema, "Kuwaona hao Wayahudi wakirudi!"

Yesu alisema, katika Mathayo sura ya 24, "Wakati mtakapouona mtini ukichipua matawi yake." Mtajua la kutazamia, mnaona, Wayahudi wakirudi!

55 Sasa, nina maoni machache yaliyoandikwa hapa. Ningetaka kuyapitia. Basi, sasa, nita—nitachukua wakati wangu, ili kwamba ninyi pia mweze kuyaandika. Sasa, haya yote

yanatukia, haya. . . Sasa sisi. . .Katika wakati tunaoishi sasa, haya yote yanatukia kwa nanii. . .Ni ya Wayahudi; hayana uhusiano wo wote na Kanisa, hata kidogo. Cho chote kutoka Ufunuo sura ya 3, hadi ya 19, hakina uhusiano wo wote na Kanisa. Huwezi kulifanya litokee sawa. Haliko hapo tu.

56 Sasa ninataka kuelezea jinsi nilivyopata jambo hili. Sasa, kwenye ubao, wengi wenu mtaona ya kwamba nimechora, nikatenga nyakati, jinsi ambavyo hilo huingia kwenye nafasi, ili kwamba lifanywe hivi kwamba kila mtu anaweza kuelewa. Mnaweza. . .Hamwezi kuona kutoka huko nyuma, nadhani, mwandiko ni mdogo sana. Na huo ni mwandiko wa Becky. Nilifikiri. . . Na, picha hiyo, nilikuwa nimechora moja mbaya kuliko hiyo. Lakini, Becky aliichora hiyo, ya ile sanamu ya ndoto ya Nebukadreza. Nami nafikiri inaonekana zaidi kama msichana, Becky, kuliko ya mwanamume. Lakini, hata hivyo, ita—itatoa maelezo, yale tunayotaka.

57 Sasa, kama tukisoma katika Biblia ya kwamba kuna majuma sabini yaliyokusudiwa juu ya watu, sasa, ile. . .hayana uhusiano wo wote na Kanisa. Yale majuma sabini hayana uhusiano wo wote na Kanisa. Kama ukiangalia hapa, kwenye jedwali hii, nimeweka wakati wa kanisa kati ya majuma hayo sabini.

58 Tunalo hapa. Ndugu fulani huko Georgia alituchorea hilo hapa, tulipokuwa tukipitia zile nyakati za kanisa. Nasi tuna hakika tunaweza kuelewa maana ya jambo hili. Huu weupe katika kanisa hapa, hiyo ina maana kwamba lote lilikuwa ni la kimitume. Na halafu katika wakati wa pili wa kanisa, walikuwa na fundisho la Wanikolai, ama, walikuwa na matendo ya Wanikolai; hayakuwa yamefanyika fundisho. Wakati wa tatu wa kanisa, likawa ni fundisho. Na katika wakati wa nne wa kanisa, likaunda madhehebu, na ilikuwa ni upapa wa Kirumi. Na katika—katika wakati wa nne wa kanisa, huo ulikuwa ni zile zama za giza.

Unaona, giza lote kule linawakilisha Unikolai, ama Urumi. Ile sehemu nyeupe inamwakilisha Roho Mtakatifu, Kanisa. Na, kwa kuwa lilikuwa lianze kwenye zamani za Mtakafitu Paulo, Kanisa lote la kimitume lilijazwa na Roho Mtakatifu. Ndipo matajiri wakaanza kuingia. Ndipo hatimaye wakaungana na kufanya kanisa jipya kabisa kutoka kwa hilo. Na ndipo hilo kanisa dogo tu likachomwa moto, na likapigwa kwa mawe, na kulishwa kwa simba, na kila kitu.

59 Katika yale matengenezo akaja Luther, mwanga zaidi kidogo, mnaona. Katika siku za Wesley, ukaingizwa mwanga mwingi zaidi tena. Lakini katika wakati wa mwisho wa kanisa hapa, ule wakati wa kanisa la Wanikolai, huo ndio wakati ambao sisi. . .Si wa Wanikolai, lakini wa Laodikia, huo ndio wakati tunaoishi. Unaona, hamna Mwanga mwingi sana.

60 Mtu fulani, wakati walipoona mchoro wake pale, alisema, “Jionee aibu, Ndugu Branham! Wakati huu mkuu wa mwangaza!”

Nikasema, “Ningedhania, utakapochujwa kweli kweli...” [Ndugu Branham anatulia—Mh.] “Hilo hata halielezi hali ya mambo ilivyo; wakati utakapopata wale walio na moyo msafi kweli, waliozaliwa kwa Roho.” Kumbukeni, huu ulikuwa ndio wakati pekee wa kanisa ambao Kristo alikuwa ametupwa nje ya Kanisa Lake Mwenyewe, wa zote hizo. Tuna kukiri kwingi sana, lakini je! tuna umilikaji, ndio tunaonena habari zake. Kristo kweli yumo kanisani? Watakuwa katika uchache sana.

61 Sasa, hebu na tuelezee yale Majuma Sabini ya Danieli kwa ufupi. Sasa huenda nikarudia hapa usiku wa leo tena; wahudumu wa Injili, kama msipokubaliana na jambo hili, ni vema. Yamegawanywa katika vipindi vitatu, kama tunavyoona katika Danieli 9. Vipindi vitatu. Kwanza, kipindi cha majuma saba; halafu na makumi sita na mbili, ambayo ni sitini na mawili; halafu kipindi cha juma moja. Yamegawanywa katika vipindi vitatu mbalimbali.

62 Sasa, nimeyagawanya hapa kwenye ubao. Kipindi cha kwanza; kipindi cha pili; na nijuavyuo mimi, kwa Injili, kwa Roho Mtakatifu, ya kwamba, wakati wa mwisho, Mungu anamrudia tena Myahudi.

63 Sasa, tunajua, kwa Injili zote, ambazo Paulo alifundisha, na hao wengine, ya kwamba Mungu atamrudia tena Myahudi. Vema, basi, kama Yeye atamrudia tena Myahudi. Tunawezaje kuliweka jambo hilo huko nyuma katika wakati wa Danieli? Hatuna budi kulitumia katika wakati huu wa mwisho. Na ni baada ya Kanisa la Mataifa kuondoka, maana Yeye huwashughulikia Israeli kama taifa, sisi tunashughulikiwa kama mtu binafsi.

64 Sasa. Nina maandishi yameandikwa hapa ambayo ningetaka kuwasomea tunapoendelea. Sikiliza:

> ...*tangu kuwekwa amri ya kutengengeza na kuujenga upya Yerusalemu*...

Ambapo, ilikuwa ni tarehe 14 mwezi wa Marchi. Kama ye yote wenu akitaka kuandika hayo, katika Kiebrania utakuta unaitwa *N-i-s-a-n*, *Nisan*, ambalo maana yake ni “Marchi.” Amri ilitolewa katika tarehe 14 ya Marchi, 445 K.K., tangazo lilitolewa kulijenga, kulijenga upya hekalu. Mnafahamu jambo hilo, kwa kuwa ninyi watu mmesoma Maandiko hayo. Mpaka lilipokamilika, ilichukua miaka arobaini na tisa kumalizia lile hekalu pamoja na mji, kuujenga upya. Na kama vile Biblia ilivyosema hapa, Danieli akinena, ama yule Malaika akimwambia Danieli, ya kwamba:

> ...*kuta*, na zitajengwa *katika* wakati wa *nyakati* za taabu.

Na wengi wetu wanakumbuka, wakati lilipojengwa, walijenga huku wameshika mawe ya chokaa katika mkono mmoja na mkono mwingine upanga, wakiangalia adui. "Na ungejengwa katika nyakati za taabu."

65 Kwa hiyo, hapa ndipo ninapopata hizo, ninapopata siku zangu. Sasa, tuna ninii mbili, kalenda tatu tofauti. Sasa tunarudi kwenye ile kalenda ya kale ya elimu ya nyota, na tunaona ya kwamba katika kalenda ya Julia kuna siku mia tatu na sitini na tano na robo moja ya siku katika mwaka mmoja. Wanapima hizo kwa kupita kwa Sardis na nyota mbalimbali, na kadhalika. Waliupima. Sasa tunaona, katika kalenda ya Kirumi ambayo ndiyo tunayotumia siku hizi, siku mia tatu na sitini na tano katika mwaka, kwa kalenda hiyo. Lakini katika kalenda ya Kikristo, ama ya kinabii, tunaona ya kwamba kuna siku mia tatu na sitini tu katika mwaka. Sasa, unaweza kushangaa mchafuko huo ulitokea namna gani.

66 Sasa, hili naweza kulisema tu kama mimi mwenyewe ninayenena. Ninaamini ya kwamba kule nyuma kabla ya yale maangamizi ya kabla ya wakati wa gharika, huko nyuma katika siku za Ayubu, na kadhalika, kwamba wao waliangalia majira kwa nyota. Nasi tunafahamu, ama huko nyuma kabla ya wakati huo, ya kwamba dunia ilisimama wima sawasawa. Halafu kwa dhambi za mwanadamu, kule kuangamizwa kwa dunia, nayo ikainama na mafuriko yakaja, kwa hiyo tuna ile mito mikuu ya barafu, na kadhalika, na upande wa juu na wa chini wa dunia umejaa barafu. Tunajua jambo hilo. Nayo dunia haisimami wima sawasawa. Imeinama. Jambo hilo liliitikisa likaitoa ambapo mwezi na nyota, ambazo ndizo walizokuwa wakiangalia, nao ndipo wakaziweka mahali pengine. Ama—ama, hungeweza kujua saa kwazo tena, kwa sababu imeinama, imeinama upande wa nyuma. Kwa hiyo, haingezipata hizo nyota katika wakati ule ule, kwa sababu ha—haiko kwenye mstari wa hizo nyota. Mnaelewa? Ninaamini hivyo ndivyo ilivyo.

67 Imeinama nyuma katika hali hiyo. Na jambo hilo linaonyesha tu ya kwamba hiki ni kipindi tu cha wakati. Hamwezi kuona? Mungu hana mambo yaliyovurugika. Anaiachilia tu iendelee namna hiyo kwa kitambo kidogo. Nami ninaamini kabisa ya kwamba jambo hilo lilifanyika.

Na katika siku hizi za mwisho ndipo Mungu atakapofunua siri hizi kwa Kanisa. Yeye hajafanya jambo hilo hapo kabla. Na sababu Yeye hakulifanya hilo, ni kulifanya Kanisa likeshe na kuomba wakati wote, likiwa halijui ni wakati gani jambo hilo lilikuwa likija. Lakini mnakumbuka, katika Danieli 12, Yeye alisema, "Wenye hekima watafahamu katika ninii ya mwisho, katika siku hii ya mwisho." Unaona? Amepewa ufunuo.

68 Roho ya hekima inaingia ndani ya Kanisa, kulijulisha Kanisa, kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu, kulileta Kanisa na

kufunua kwamba tunaishi katika siku gani. Jinsi ile ile tu Gabrieli alivyokuja kwa—kwa Danieli, Roho Mtakatifu analijia Kanisa katika siku za mwisho, kufunua mambo hayo makuu ya siri, yenye kilindi. Mnaelewa sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”]

69 Basi, hilo lingetupilia mbali huo mwaka wa elimu ya nyota ama mwaka wa Julia, kalenda, unaona, mwaka wa mwashi, kwa sababu dunia inalala upande. Sote tunajua jambo hilo, kwa kusoma shuleni. Na imevurugika, kwa hiyo, wao hizo nyota, hazingepita kwa mstari mmoja pamoja na dunia wakati ule ule. Kwa hiyo, kalenda ya Kirumi imekosea, pia, kwa sababu huwezi kuweka siku pamoja. Kuna mambo mengi tu ambayo ningeweza kusema papa hapa. Ya kwamba tunaona, hata kwa maumbile yenyewe, yanatufundisha kuna siku thelathini tu katika mwaka.

70 Sasa, hebu tuchukue Ufunuo ambapo itatubidi kwenda hapa katika zile zama za wale manabii wawili. Biblia ilisema, “Walitabiri siku elfu na mia mbili na sitini.” Sasa, hebu chukua kalenda ya elimu ya nyota, itakosea kwa mbali kutoka hesabu ya miaka mitatu na nusu. Na ukichukua kalenda ya Kirumi tuliyo nayo siku hizi, itakosea kwa mbali. Lakini chukua kalenda ya kinabii, na kuna siku elfu na mia mbili na sitini kamili, kwa siku thelathini kwa mwezi. Unaona?

71 Tuna siku thelathini katika miezi mingine, thelathini na moja katika mingine, ishirini na nane katika mingine. Mnaona, sote tumechanganyikiwa. Lakini Mungu haruki-ruki, juu chini, huku na huko. Yeye hugonga jambo lile lile barabara. Naam, bwana. Lilo hilo kabisa, siku thelathini katika mwezi; si thelathini na moja, halafu thelathini, kitu kingine. Mnaona? Lakini jambo hilo lilifanywa katika uchumi mkuu wa Mungu, kuliweka kanisa likikesha na kuomba, mpate kusafisha nguo zenu katika Damu ya Mwana-Kondoo. Lakini, loo, katika siku hizi za mwisho, Yeye aliahidi! A-ha. Sasa tunaona mahali tunapoishi. Sasa, kumbukeni, lile kusudi, kusudi pekee, ni kufanya jambo hili.

72 Sasa, kama kulikuweko na saba . . . Angalia, kuna siku arobaini na tisa kamili . . . miaka arobaini na tisa, hasa, katika ule wakati wa kulijenga lile hekalu. Yale saba, ni majuma saba ya kinabii, majuma saba, maana kuna majuma saba yaliyokusudiwa kwa ajili ya hekalu, kulijenga hekalu. Na lilijengwa kwa miaka arobaini na tisa kamili. Sasa tuna maana ya wakati wa majuma, maana kama Biblia ilisema, na yule Malaika alisema, ilichukua majuma saba mpaka kujengwa kwa hekalu. Na ilichukua miaka arobaini na tisa kamili kulijenga hilo hekalu, kutoka—kutoka tarehe 14 Marchi mpaka 5-538 K.K. Mpaka lile hekalu lilipojengwa upya, na barabara zikajengwa upya, miaka arobaini na tisa kamili. Kwa hiyo, tunapata nini? Tunapata nini? Kwa kuwa, kama majuma saba yanamaanisha miaka arobaini na tisa, basi juma moja ni sawa na miaka saba.

Na saba mara saba ni arobaini na tisa. Hiyo ni barabara kabisa. Haya basi.

73 Kwa hiyo sasa hakuna kukisia jambo hilo. Tunajua sasa ya kwamba kila juma lilimaanisha miaka saba. Mmelipata? Hebu na tuliseme jambo hilo pamoja. [Ndugu Branham na kusanyiko wanasema pamoja—Mh.] "Juma moja ni sawa na miaka saba." Sasa tunajua tumelipata. Juma moja ni sawa na miaka saba.

74 Tumelipata papa hapa, juma la kwanza. [Ndugu Branham anaelekeza kwenye mchoro ubaoni—Mh.] Miaka arobaini na tisa mpaka kufikia kule kujengwa upya kwa hekalu. Sasa, mstari huu wa juu hapa unawakilisha taifa la Kiyahudi linapopita. Huu ni wakati tu. Na wakati unaposhuka hapa chini, unashuka unatoka katika taifa la Kiyahudi, kuingia katika wakati wa Mataifa. Halafu unapanda juu tena na kuwashika Israeli, na unaendelea.

75 Sasa, Mataifa hawakugawiwa wakati wo wote ule. Ilisema tu, "Wakati wa Mataifa." Nasi tunaona, hata Yesu hakuwagawia wakati. Kwa maana tunaona hapa nje, katika Luka 21:24, Yeye alisema, "Watazikanyaga kuta za Yerusalemu hata Ninii ya Mataifa . . . " Hebu ninukuu jambo hilo. Ninalinukuu tu jambo hilo kutoka kichwani. Hebu nilisome, kwa sababu litakuwa kwenye kanda hapa, nasi tunataka kuwa na hakika ya kwamba tutalipata sahihi. Vema, kama mnataka kufungua hapo pamoja nami, katika Luka 21:24. Nilisoma jambo hili dhahiri, vizuri nilivyoweza.

> *Wataanguka kwa ukali wa upanga, nao watatekwa na kuchukuliwa . . .*

Anazungumza habari za akina nani? Wayahudi. Huko ilikuwa ni kule kuangamizwa kwa lile hekalu, katika 70 B.K.

> *. . . nao watatekwa nyara na kuchukuliwa katika mataifa yote; . . .*

Sasa kumbuka, si tu huko chini huko tu Babeli, si huko Rumi tu, lakini "kwa mataifa yote." Huko ndiko Wayahudi waliko leo, "mataifa yote."

> *. . . na Yerusalemu utakanyagwa na Mataifa, hata majira ya Mataifa, yatakapotimia.*

76 Basi, kuna wakati uliopangwa, lakini hakuna mtu ajuaye utakuwa ni lini. Mnaona? Ni siri, unaona, wakati wa Mataifa. Lakini, Wayahudi . . . Halafu, hatuwezi kujua wakati kwa mambo ambayo Kanisa, kama limerudi nyuma ama linaendelea, ama linafanya nini. Huwezi kujua kwa njia hiyo. Lakini, waangalie Wayahudi, hiyo hapo kalenda ya wakati. Mnaona jambo hilo? Mungu aliwapangia siku, saa, na wakati kamili, lakini hakuwapangia Mataifa hata kidogo. Aliwapangia Wayahudi, kwa hiyo hebu na tuwaangalie Wayahudi, ndipo tutaona mahali tulipo.

77 Basi, sasa, yale majuma saba yalikuwa ni miaka arobaini na tisa. Tumelipata dhahiri sasa, ya kwamba juma moja ni—juma moja ni miaka saba; juma moja, miaka saba.

78 Sasa tunaambiwa, "Tangu kuwekwa amri . . ." Sasa, hapa ndipo shida inapoingilia. Sasa tunaambiwa:

> . . . *tangu kuwekwa amri ya* kuujenga upya mji hata zamani za Masihi (na Masihi alikuwa Kristo, bila shaka) *kutakuwa na majuma saba, na majuma sitini na mawili*: (ikifanya majuma sitini na tisa) . . .

Mnaona? Vema. Na saba mara tisini na tisa inafanya miaka mia nne na themanini na mitatu. Sasa, mnayaandika? Kama mkitaka niyarudie tena, nitafurahia kufanya jambo hilo.

79 Sasa tunaambiwa, "Tangu kuwekwa amri ya kuujenga upya mji, hata zamani za Masihi, kutakuwa na saba," (saba, hiyo ni ya kwanza—ya kwanza, papa hapa) "majuma saba, na sitini na mawili," inafanya, sitini na mbili na saba ni sitini na tisa, majuma sitini na tisa. Saba mara sitini na tisa ingefanya miaka mia nne na themanini na mitatu. Kwa hiyo, mpaka zamani za Masihi . . . Sasa tunakaribia sehemu *hii* hapa. Mpaka Masihi, hakuna budi kuwe na miaka mia nne na themanini na mitatu, miaka mia nne na themanini na mitatu.

80 Basi, sasa, Yesu, Masihi, aliingia mji wa Yerusalemu kwa shangwe, amepanda nyumbu mweupe, Jumapili ya Mitende, tarehe 2 Aprili, 30 B.K. Yesu aliingia Yerusalemu katika Jumapili ya Mitende, 30 B.K. Na sasa, tangu 445 K.K. hadi 30 B.K., ni miaka mia nne sabini na mitano kamili.

81 Lakini, kama tulivyokwisha kuona tayari, ya kwamba yale majuma sitini na tisa yanafanya miaka mia nne themanini na mitatu. Sasa, hapo ndipo shida inapoingilia, papo hapo. Unaona? Tunaninii tu, kwa alama ya Biblia hapa, wakati, ni miaka mia nne na sabini na mitano tu. Na, kwa kweli, ni miaka mia nne na themanini na mitatu, tofauti ya miaka minane.

82 Sasa, Mungu hawezi kulifanya likosee. Kama Yeye alisema ingekuwa ni siku kadha, ni siku kadha. Kama akisema ni kiasi fulani, ni kiasi fulani. Kwa hiyo tutafanya nini? Sasa, ile 475 K.K. hadi 30 B.K., ni miaka ya Julia ama ya elimu ya nyota, ambayo ni siku mia tatu na sitini na tano na robo ya siku—katika kila mmoja. Lakini wakati tunapozibadilisha siku hizo zikawa za kalenda yetu ya kinabii . . .

83 Sasa hebu nisimame papa hapa kwa dakika moja. Mpate kujua bila tashwishi yo yote, nisingeweza kuchukua mahali hapa pamoja tu. Ninaweza kulipitisha katika Maandiko yote na kuwathibitishia ya kwamba siku saba ni hayo saba, juma moja ni—ni miaka saba, katika Biblia. Nimeisha lithibitisha sasa hivi tu hapa, katika Ufunuo sura ya 13, ama sura ya 11 na aya ya 3. Hao manabii watatabiri siku elfu mia mbili na sitini, ambazo ziko katikati ya lile juma la mwisho la Wayahudi, ndipo

wanakatiliwa mbali na Har-magedoni itaanza. Basi kama jambo hilo ndivyo lilivyo, hilo hapo tena, siku thelathini barabara katika mwezi. Mnaona? Basi, ni—si siku thelathini na moja na siku ishirini na nane, na kadhalika. Ni siku thelathini kamili katika mwezi, kila wakati.

84 Kalenda yetu ya kinabii inatuleta kwenye siku mia tatu na sitini, kama tunazotumia sasa katika Maandiko. Tuna mia nne na themanini na tatu kamili. Hiyo hapo, mia nne na themanini na tatu. Hapa tuna thibitisho halisi la huo unabii, ukweli halisi. Kwa kuwa, tangu kuwekwa amri ya kulijenga hekalu, hata kuangamizwa kwake, wakati walipomkataa Kristo na kumwua katika mwaka wa 33 B.K., wakati Kristo alipouawa, ni miaka mia nne na themanini na mitatu kamili.

Sasa, tangu kuwekwa amri ya kuujenga upya Yerusalemu, yalikusudiwa majuma saba, ambayo yalimaanisha ni miaka arobaini na tisa. Na miaka arobaini na tisa ilitimia kikamilifu. Vema, tangu kujengwa upya kwa hekalu hata zamani za Masihi, ilikuwa ni miaka mia nne thelathini na minane. Hivyo, miaka mia nne na thela- . . . miaka mia nne thelathini na minne. Na miaka mia nne na thelathini na minne (wakati), arobaini na tisa, inafanya miaka mia nne na themanini na mitatu. Ilitimilika kikamilifu, kwenye siku yenyewe kabisa, kutoka siku baada ya siku. Amina! Sawa kabisa.

85 "Masihi aliye Mkuu atakuja." Mnaona? Saba mara sitini na tisa ni miaka mia nne na thela- . . . na—na themanini na nne hasa. Kweli kabisa, imetimia kamili kabisa. Kwa hiyo, basi, tunajua kikamilifu, tunajua barabara hasa, ya kwamba Maandiko hayo ni sahihi. Haya hapa. Lakini, unaona, yote haya . . .

86 Wakati Mungu alipokuwa na ulimwengu uliotangulia zamani za ile gharika na kuuangamiza kwa maji, na kubadilisha ile tarehe ya elimu ya nyota; ndipo akawaacha Warumi waingie na kuanzisha kalenda yao wenyewe, ambayo hiyo hugonga na kuruka, na kadhalika. Nami nadhani, ya kwamba, hata katika ile ensaiklopidia niliyokuwa nikisoma.

87 Aisee, jambo lingine, Ndugu Kenny Collins, je! yeye yumo jengoni asubuhi hii ya leo, Kenneth Collins? Unajua wakati uliponitumia lundo hilo kubwa la kamusi? Unakumbuka jambo hilo? Ulinitumia kule karibu roli zima la hizo. Nikawazia, "Mjinga kama mimi ningefanya nini na hizo zote?" Unajua, Bwana alikuwa akikuongoza, Kenny. Humo ndimo nilimopata zile habari, mumo humo kutoka kwenye ensaiklopidia hiyo ya kale, "lile neno wakati," nami nilikuwa nikisoma. Na Becky huzitumia shuleni kwake. Ninazo kwenye chumba changu cha kujisomea, huko katika chumba changu cha faragha kwenye orofa ya chini. Basi tulishuka tukaenda kule na tukaichukua, na tukalichunguza humo, na kulipata, naam, katika kalenda zote na wakati ambao umewahi kuwepo. Mnaona? Kwa hiyo, tulilipata.

88 Hilo hapo, sawa kabisa, miaka mia nne na themanini na mitatu. Tangu kuwekwa amri ya kutengeneza ninii—kutengeneza lile jengo, hata zamani za kukataliwa kwa Mashihi aliye Mkuu inafanya miaka mia nne na themanini na mitatu kamili, kwa kalenda.

89 Sasa unaona, sisi tukitumia kalenda ii hii papa hapa. Kwa sababu, kama Mungu alitumia kalenda hii hapa, basi hana budi kuitumia wakati mwingine wote katika Biblia nzima. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu habadiliki. Kwa hiyo, kama majuma saba yalikuwa ni miaka arobaini na tisa, majuma saba tena ni miaka arobaini na tisa. Juma moja ni miaka saba, unaona, kwa hiyo inakuwa ni sahihi kabisa. Na kama ilitimia kikamilifu kabisa pale, itatimia kikamilifu tena. Amina! Loo, jamani! Hilo linanichangamsha kabisa. Loo, na—napenda—napenda kujua jambo ninalozungumzia. Na—na—napenda jambo hilo.

Kwa sababu, kama alivyosema maskini yule mzee, huko chini Kentucky, aliniambia, kasema, "Ninapenda mtu fulani azungumze, ambaye anajua analosema."

Nikasema, "Mimi niko hivyo, pia."

Akasema, "Hiyo ndiyo shida yenu ninyi wahubiri, hamjui yale mnayozungumzia."

90 "Vema," nikasema, "ninathamini matamshi yako, lakini kuna mambo tunayozungumzia ambayo tunayajua." A-ha. Hiyo ni kweli. Ninajua ya kwamba nimezaliwa mara ya pili. Ninajua ya kwamba nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Najua kuna Mungu, kwa maana nimezungumza Naye.

Yeye amepata kunena kupitia kwangu, na kunena nami, na kuzungumza na wengine, na kuniambia habari za wengine. Nami ninajua ya kwamba Yeye ni Mungu. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa mwema sana hata akashuka na kuniruhusu nipigwe picha pamoja Naye, ambapo ulimwengu wa kisayansi hauwezi kukanusha jambo hilo. Nami nikafungua Maandiko na kuona hiyo ni kuutimiza kabisa wakati huu wa kanisa, yale yanayotukia hasa, kwa hiyo ninajua ya kwamba tuko hapa. Amina.

91 Sasa, huenda tusiwe na elimu. Huenda tusiwe watu wa tabaka la juu, na vitu kama hivyo. Huenda tusiwe watu mashuhuri, lakini tunamjua Mungu. Tunamjua kwa sababu kuna Roho Mtakatifu, mnaona, na Yeye analingana na Neno kwa Neno katika Maandiko, ndipo tunajua ya kwamba ni kweli. Tunaishi katika siku za mwisho.

92 Sasa, hapo, kumbukeni sasa, hilo, mwaka huu wa kinabii, wa siku mia tatu na sitini kwa mwaka. Angalieni vitu vingine vyote. Viumbe, iwapo baadhi yenu ninyi watu mnaweza kuelewa, hata kwa wanawake, na kadhalika. Mnaona? Thelathini, siku thelathini, hebu angalia tu hilo—ni ninii. . . Viumbe vyote

vimewekwa namna hiyo. Mnaona? Si thelathini na moja, thelathini, ishirini na nane ama kitu fulani. Ni siku thelathini kamili. Kwa kila mwaka, hiyo ni kalenda ya kinabii, siku mia nne themanini na tatu.

93 Hapo tuna thibitisho halisi la ule unabii, miaka mia nne na—na arobaini na mitano, kabla, ilikuwa ni sahihi kabisa. Sasa, yote hayo yalitabiriwa yangetimia. Na majuma hayo sabini hayakutimia wakati huo, kwa hiyo yameachwa kwa ajili ya siku za mwisho sasa.

94 Sasa, enyi ndugu zangu wa Kipentekoste; sasa, ndugu zangu Mashahidi wa Yehova; mnatambua? Mnajua mahali ambapo wale mia na arobaini na nne elfu walipotokea? Mnajua mahali miujiza yote ya Ufunuo ilipotokea? Huko kwenye wakati wa Kiyahudi, si katika wakati wetu. Hakuna jambo lililorekodiwa ndani yake, ni Kanisa tu kujitayarisha na kuondoka. Hakika, pamoja na nguvu za Mungu, tunafanya miujiza na mambo makuu. Tunajua jambo hilo. Lakini jambo lenyewe lilikuwa hapa kwa Wayahudi; ninamaanisha, nguvu halisi, za kutenda kazi, za kutenda miujiza. Wale ninii nne . . .

95 Wale mia na arobaini na nne elfu hawaonekani pale. Wao wako huko . . . Hawaonekani katika sura ya 3. Wao wako huko mbele katika Maandiko, mbele zaidi. Na sasa tunaona ya kwamba mambo haya yote ambayo yalikuwa yatendeke, yalikuwa ni huku kwenye kipindi hiki cha juma la sabini, juma la mwisho. Sasa, kama tayari wamekwisha kuwa na majuma sitini na tisa, na wakayaishi sawasawa tu na vile Mungu alivyosema watayaishi, na ikatukia sawasawa kabisa na vile Mungu alivyosema ingetukia, basi kuna juma moja zaidi lililoahidiwa Myahudi. Sasa, ndugu, iweni tayari tu. Mnaona? Mnaona? Sikilizeni jinsi tulivyokaribia. Juma la mwisho, saba, mwaka wa saba.

96 Sasa, kila mtu anaelewa kufikia umbali huu, kama mnaelewa? Kila mtu anaelewa umbali huu, ya kwamba hiyo ni Kweli kabisa. Ni Biblia. Ni miaka ya kinabii.

97 Sasa tumefikia, na tukafikia hapa kwenye kule kukataliwa kwa Masihi, unaona, kutoka kwenye ninii . . . hadi kukataliwa kwa Masihi, lile juma la mwisho.

98 Sasa, ninataka kusimama papa hapa kwa muda kidogo na kuelezea jambo hili. Ya kwamba, wakati walipomkataa Masihi, ilikuwa ni wakati ambapo wao, bila shaka, walimkataa Yesu kama Mwokozi, na kumsulibisha. Kumbukeni hapa vile ilivyosema Biblia, "Naye atakatiliwa mbali, bali si kwa ajili Yake, Masihi, aliye Mkuu." Sasa wazia jinsi unabii huo ulivyotimilika kabisa. Ninataka kusisitiza jambo hili kwenu. Ya kwamba, kama unabii huo ulitimia kikamilifu kwenye ile tarehe, barabara kwenye ule wakati, na ni vile vile kabisa ilivyosemwa unabii huo ungetimia; huu mwingine wa saba, huu mwingine wa

majuma saba yaliyosalia . . . moja la miaka saba, hasa, (siku saba: miaka saba), utatimia vile vile hasa kulingana na Maandiko.

99 Sasa kumbukeni, Yeye alikatiliwa mbali, Masihi. Wayahudi, Mungu alikoma kuwashughulikia. Hawakuendelea mbele zaidi. Halafu wakatawanywa na Dola ya Kirumi. Na, halafu, kama ukiangalia kwenye jedwali yangu hapa, nawataka mpate jambo hili sasa na kulichora. Mnaona hapa ambapo nimeweka msalaba? Hapo ndipo wao walipokataa. Lakini saa ilisonga mbele kwa muda kidogo tu kuhusu jambo hilo, mnaona. Kwa nini? Thelathini, arobaini, hamsini, sitini, sabini. Miaka arobaini baadaye, Tito, yule jemadari wa Kirumi, aliiangamiza Israeli, Yerusalemu, na kuwatawanya watu hao kila mahali ulimwenguni. Mnaona, Tito, miaka arobaini baadaye. Kwa hiyo, kwa kweli, wakati wa Kiyahudi uliendelea hata ninii yote . . .

100 Mungu hakuwa akiwashughulikia. Yeye aliwashughulikia tu mpaka walipomkataa Kristo. Basi walipomsulibisha Kristo, wao walipaza sauti, "Damu yake na iwe juu yetu na juu ya watoto wetu," na imekuwa hivyo tangu wakati huo. Lakini kabla hawajatawanyika . . . Sikilizeni! Loo, ndugu! Kabla hawajatawanyika kila mahali ulimwenguni, ilimchukua Mungu kama miaka arobaini kulibomoa lile hekalu na kuwatawanya kila mahali ulimwenguni. Lakini Mungu alishindwa kuwashughulikia tena. Mungu alishindwa kuwashughulikia tena.

Yeye alienda kushughulika na Mmataifa. Mnajua jambo hilo, mnalielewa sasa? Sasa, hapa tunaanza katika nyakati za kanisa, majira ya Mmataifa, Mungu akiwaacha Wayahudi.

101 Sasa, ndugu yangu mmishenari, mambo hayo yalikuwa kwa—kwa—kwa Wayahudi, ndugu wa thamani hapa mahali fulani. Hapa ndipo ninakutaka ushike na ufahamu. Unaona, Mungu aliacha kuwashughulikia Wayahudi papo hapo, kwa sababu Mungu daima huwashughulikia Israeli kama taifa. Sote tunajua ya kwamba Israeli ni taifa. Mataifa ni watu, na ilimbidi Yeye kuchukua watu kutoka kwa Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake. Tutafikia jambo hilo mnamo dakika chache.

102 Lakini sasa, katika hizi nyakati saba za kanisa ambazo tumepitia, katika wakati wa Mmataifa, tangu kusulibiwa kwa Kristo mpaka mwisho wa nyakati za kanisa. Sasa hilo tumelipatia. Tumelipitia, lote. Sasa tunafikia mahali ambapo tunaweza kuliingilia jambo hili, tuingie kwenye ile Mihuri Saba, vile Vitasa Saba, Baragumu Saba, na yote hayo, na tuyaweke pamoja; yote inanahusiana na Wayahudi, na hukumu ya Mungu kwa watu walio juu ya nchi. Na wale masalia . . .

103 Kumbukeni, katika wakati huu mkuu wa mateso, kuna mamilioni ya Mataifa watakaokufa katika mateso hayo. Huyo bibi-arusi aliyekataliwa, hao—hao masalia ya uzao wa mwanamke, wanawali waliolala, yeye anapitia hayo moja kwa

moja. Ni—ni dhahiri tu kama haya majuma sabini; dhahiri tu. Nao watapitia kwenye jambo hilo. Kwa hiyo, kama huna Roho Mtakatifu, afadhali uingie Kwake upesi uwezavyo. Tuko wakati wa mwisho.

104 Sasa angalia, nyakati saba za kanisa. Sasa, haitanilazimu kuzipitia, kwa sababu tunazo kwenye kanda, na zinawekwa kwenye vitabu na kila kitu. Huo, huo ulikuwa ndio wakati ule ambao Mungu hakusema kabisa kungekuweko na kiasi kadha cha siku fulani, cha masaa kadha, ama cha miaka kadha; Yeye hakusema lo lote. Alisema, "Mpaka wakati wa mataifa utakapotimia." Kasema, "Mpaka!" Kuta zitakanyagwa hata Mungu atakapokoma kuwashughulikia Mataifa.

105 Sasa, tunaona, ya kwamba wakati wote katika nyakati hizi, temeona Roho Mtakatifu aliingia. Ndipo Mungu, huko nyuma hapo mwanzo, akaanza kuwaambia, kwenye kukataliwa kwa Kristo, Mungu alimwonyesha Yohana sawasawa kabisa mambo ambayo yangetukia katika enzi ya Mataifa. Sasa, unaona, hatuna wakati wo wote uliopangwa, kama Wayahudi, lakini tuna ishara. Tunaninii—tuna nguzo ya kuonyesha njia. Vema, Mungu alishughulika na Wayahudi sawasawa kabisa tu na vile alivyosema Yeye angefanya katika hiyo miaka sitini na tisa, ama, ilikuwa miaka mia nne na themanini na mitatu, lakini majuma sitini na tisa. Na juma moja lilibakia, juma moja lingali limekusudiwa.

106 Sasa, hatuwezi kuliingiza *hapa* ndani, maana hili ni la Mmataifa, Kanisa hili. Sasa, ni wangapi wanafahamu jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, hii ni Ufunuo, kuanzia kwenye sura ya 1, mpaka sura ya 3 unatupeleka kwenye Laodikia. Sasa, tunaona barabara jinsi vile hasa ilivyokuwa kwa kanisa lote, Kanisa lenyewe la ulimwengu. Mungu kamwe hakumhusisha mwenye dhambi, yeye alininii tu. . . isipokuwa kama alitaka kuokolewa. Lakini, ulimwengu wote wa Kanisa ulikuwa mweupe; ndipo wakaja Wanikolai ambao walitaka kuunda madhehebu. Watu mashuhuri wakaingia nalo. Hii ilikuwa huko Nikea, Rumi, wakati walipokuwa na Baraza la Nikea. Nao walifanya nini? Walilifanya kanisa kuwa madhehebu, ndipo wakaanza kuwatesa Wakristo. Halafu, katika wakati uliofuata wa kanisa, Ukristo, katika hali ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, ulikuwa karibu sana kufutiliwa mbali.

107 Lakini basi, kwamba ninyi watu mnajua, ya kwamba nilirudi nyuma na kuchukua historia, *Nicene Fathers*, na *Pre-Nicene Fathers*, na historia yote ya Kanisa, na magombo ya kale sana ambayo ningeweza kupata, na kila moja ya hayo yaliwathibitishia ya kwamba Kanisa ambalo Mungu alikuwa akinena habari zake halikuwa ni hilo kanisa Katoliki lililounda madhehebu wala madhehebu mengine yo yote. Mungu alikuwa akizungumza habari zake, na hizo nyota zote kuu za zama hizo, ilikuwa ni watu waliofundisha ubatizo wa

Roho Mtakatifu, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, na kule kuja kwa Roho wa Mungu, na—na kunena kwa lugha, na kufasiri lugha, na kuponya, na miujiza, na ishara. Hilo ndilo Mungu analoshughulika nalo. Hawezi kubadilisha nia Yake, aseme, "Vema, hivi ndivyo ninavyotaka Kanisa liwe, Kanisa la kimitume; sasa nia Yangu ni kuwa na Kanisa la kiungwana." Mungu habadiliki! Angali ni Roho Mtakatifu.

108 Nasi tunaliangalia na kulileta, basi, tunapoona tabia ya Mungu na yale Yeye. . . kisha tunayaelezea Maandiko. Ndipo tunachukua hi—historia inayoonyesha kwamba hilo lilitimia kikamilifu; kikamilifu kabisa kwenye tarehe, wakati, na kwa kila kitu ambacho Mungu alisema kupitia kwa Yohana, kwamba kingetimia, kilitukia kwa wakati huo wa Mataifa.

109 Sasa, tunajikuta wenyewe, bila shaka yo yote, katika Wakati wa Laodikia. Tunajua tuko katika huo. Tumepitia wakati wa Kilutheri; tumepitia wakati wa Wesley; sasa tuko katika wakati wa Laodikia, wakati wa mwisho. Nasi tunatambua ya kwamba kila moja la makanisa hayo lilikuwa na mjumbe. Tunaona jambo hilo. Zile nyota saba mkononi Mwake, ambazo zilikuwa ni roho saba zilizotoka mbele za Mungu. Kila mmoja ulikuwa na mjumbe. Nasi tunashuka na kuona, kwa Biblia, tabia ya mjumbe huyo ingalikuwa ni tabia gani. Ndipo tunamchagua mtu katika historia, aliyekuwa na tabia hiyo. Basi tunapompata mtu huyo katika historia, ambaye alikuwa na tabia kama hiyo, tunakuta kwamba yeye ndiye aliyekuwa mjumbe wa wakati huo wa kanisa. Ndipo tunatafuta kujua ni wa Roho gani, na yale mtu huyo aliyofanya. Ndipo tunakuta kwamba alikuwa mtakatifu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, Mtakatifu Ireneo, na hao wengine wote, na—na Mtakatifu Columba, na watu wote wale waliojazwa na Roho Mtakatifu. Nasi tunajua ya kwamba, kwa Maandiko, ya kwamba Roho wa aina hiyo hana budi alikuwa katika mtu wa namna hiyo kwa ajili ya wakati uo huo. Hilo hapo, kwa hiyo haiwezi kukosea. Amina! utukufu kwa Mungu! Hili ni ninii tu. . .

110 Sijui, ndugu. Hilo linanifanyia mengi kuliko cho chote kile nijuacho, mnaona, kwa sababu ni Neno la Mungu likizungumza Lenyewe. Ninapomsikia Mungu akisema jambo, ninasema, "Amina! Hilo ni kweli. Hilo ni sawa." Mnaona? Hilo latosha. Limekwisha. "Mungu alisema jambo hilo." Hilo, hilo linatosha.

Vema, Mungu alisema ya kwamba jambo hilo lingetukia namna hiyo, nasi tumeliona katika historia na kwa Maandiko. Tungesoma juu ya wakati huu wa kanisa, mambo ambayo ungefanya, yale yangetukia, wakati huo wa kanisa ulikuwa na mjumbe wa namna gani. "Kwa—kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia. Kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi, Thiatira," haya yote mbalimbali. Kisha tunarudi katika historia na kuona yule—yule mjumbe wa kanisa hilo, na tukaona kwamba alikuwa ni

nani. Ndipo basi tulilichora, tukaweka majina yao chini yake, na ndio hao hapo. Unaona, tunajua jambo hilo lilitimia kikamilifu.

111 Sasa, nasi tunajua ya kwamba Mungu alikuwa, daima alikuwa, na daima amekuwa, na dhidi ya madhehebu ya kidini. Naam, bwana. Alisema jambo hilo. "Wanikolai, hao ndio ninaowachukia!" *Niko* maana yake ni "kuwashinda wafuasi." *Lai* maana yake, lai ni, "kanisa, ule mwili." *Niko* maana yake ni kushinda, kutiisha," kwa maneno mengine, "fanya mtu mtakatifu, mtu fulani aliye juu ya mwingine."

Sisi sote ni watoto. Tuna Mfalme mmoja, huyo ni Mungu. Tuna mmoja aliye Mtakatifu, na huyo ni Mungu. Amina! Naye yuko katikati yetu katika umbo la Roho Mtakatifu. Huyo ndiye Aliye Mtakatifu.

112 Sasa, tunashuka mpaka tunakuwa na hakika ya kwamba tukipitia katika—katika wakati huo wa Kiyahudi tuna hayo majuma sitini na tisa hasa, kwa historia, kwa kalenda, kwa mwaka wa Mungu wa kinabii, tukileta historia ya kalenda ya kinabii, tangu Agano la Kale hata kwenye lile Jipya, tukionyesha ndivyo hivyo kabisa. Mnaona?

Sasa tuna kanisa la Mataifa kutoka hapo mwanzo, hadi kufikia siku ya mwisho, nasi tunajua tunaishi katika siku ya mwisho. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara kadha—Mh.] Amina! Mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."] . . .? . . . [Ndugu Branham anapiga mimbara mara moja.] Sasa, basi, kama tunaishi katika siku hii ya mwisho, katika mwisho wa wakati huu, basi tuko wapi?

113 Angalia, huku nyuma kabisa, mnaona mstari huu uliochorwa nyuma *hapa*, ambapo Mungu aliwashughulikia Wayahudi . . . Ama, hakuwashughulikia Wayahudi hata, ilimchukua muda mrefu sana kuwapata. Ilimchukua miaka arobaini kuwafikisha katika hali ambayo angewafanya waangamizwe, kwa mataifa yote. Kila mahali, katika siku za Mataifa, ilimbidi kuwafikisha katika hali fulani kabla ya kuwatimiza Neno Lake. Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko, "Amina!"—Mh.] Wote wanaolipata jambo hilo, semeni, "Amina!" ["Amina!"] Mnaona, ninataka nihakikishe mnalipata.

114 Sasa ni jambo gani lililotukia? Angalia juu ya wakati huu wa mwisho wa kanisa. Mnaona hili ongezeko dogo? Siku za mataifa zinakwisha. Na kwa miaka arobaini iliyopita, Wayahudi wamekuwa wakirudi Yerusalemu, wakirudi kwenye nchi ya uenyeji wao. Haleluya! Mnaona mahali tulipo? Ilichukua miaka arobaini, tangu kukatiliwa kwa Masihi, mpaka wakati Tito alipoliangamiza hekalu na kuwatawanya Wayahudi. Imekuwa miaka mingine arobaini ambayo Mungu aliufanya mgumu moyo wa kila namna ya Farao kila mahali, na kuwafukuza Wayahudi warudi katika nchi ya uenyeji wao. Lakini leo wamerudi katika nchi ya uenyeji wao tena, na Kanisa liko katika wakati wa

mwisho. Amina! [Ndugu Branham anatulia—Mh.] Loo, ni—ninajaribu tu kusoma; siwezi.

115 Angalia, Wayahudi wako katika nchi ya uenyeji wao, na wamekuwa wakirudi. Kama ukipata *Decline Of the World's War*, kitabu cha pili, wakati Jemadari Allenby, baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, aliporuka juu ya Yerusalemu na kuutwaa, akauteka Yerusalemu. Na hao wanaume Wakristo wakaingia Yerualemu kwa hatua za kiaskari huku wamevua kofia zao. Ndipo Allenby akajisalimisha bila hata kufyatua risasi . . . ama—ama wao wakajisalimisha kwa Allenby, hao Waturuki. Na tangu kwakati huo, Mungu akaanza kuufanya mgumu moyo wa Mussolini, moyo wa Hitler, moyo wa Stalin, mioyo ya watu kila mahali nchini, kumchukia huyo Myahudi.

116 Halafu yale madege makubwa mno yaliyoshuka, yanayoitwa Eastern Airlines, ama Pan American Airlines, ama lo lote lile. Ninaamini yalikuwa yanaitwa TWA. Yaliandikwa kwenye ga—gazeti, gazeti la *Life*, ninaamini, *Look* ama *Life*. Ninaamini lilikuwa la *Life*. Katika miaka mitatu ama minne tu iliyopita, na Mungu amekuwa akiwafukuza Wayahudi warudi katika nchi ya uenyeji wao, ambapo wameiacha kwa miaka elfu mbili, wakati Mataifa walikuwa wakijitayarisha. Na sasa Mataifa wametoa Kristo nje ya kanisa, kulingana na Ufunuo sura ya 3. Hata hawezi kurudi katika kanisa Lake. Hana mahali pa kwenda. Amekataliwa.

117 Na ni wakati wa Kunyakuliwa. Wote waliokombolewa kupitia *hapa*, hizi nukta ndogo namna hii, ni kutwaliwa kwa watakatifu katika ule ufufuo. Unaona, sote tunakutana papa *hapa* pamoja. Biblia ilisema, "Sisi tulio hai na tuliosalia hata kuja kwa Bwana hatutawatangulia ama kuwazuia hao waliolala mauti." Kote kote kutoka *hapa*, *hapa*, na *hapa*.

118 Unawezaje, ewe ndugu Mpentekoste, unawezaje kuyaingiza huku katika Wakati wote hapa katika Kanisa la Laodikia?

Wao wako humo, wamelala, katika kila mmoja wa nyakati hizi, wakingojea. "Na sisi tulio hai, lile kundi dogo lililosalia hapa, tutakaokuwa hai hata . . . Kuja kwa Bwana hatutawatangulia hao waliokwisha kulala mauti; kwa maana baragumu ya Mungu italia, na waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza; nasi tutanyakuliwa juu pamoja nao." Amina! "Pamoja nao," sisi *hapa*, tunakutana papa *hapa*, "kwenda kumlaki Bwana hewani." Na hivyo ndivyo ilivyo hapa. Tuko wapi? Papa *hapa*. Masihi alikatiliwa wapi? Mahali pale pale ambapo Neno lilisema. Hilo juma la sabini litaanzia wapi? Mara baada tu ya Kanisa hili kukatiliwa mbali. Ndipo Mungu anawarudia Wayahudi.

119 Je! hamkumbuki, ya kwamba, mara tu Kanisa linapoondoka—Kanisa linaondoka, ndipo Wayahudi wanaendelea, wanaingia? Lakini, kwanza, jambo linalofuata

katika utaratibu, si ufufuo mkubwa sana wa taifa—ufufuo wa taifa miongoni mwa Mataifa. Jambo linalofuata katika utaratibu, ni kule kuja kwa Ufalme wa Mungu, kule Kuja kwa Kristo.

120 Sasa, kama ungetaka, tungeweza kurudi nyuma hapa sasa katika Danieli mlango wa 2, kifungu cha 34 na 35. Na wakati Danieli alipopewa . . . Mlango wa 2, kifungu cha 34 na 35, wakati Danieli alipokwisha kupewa lile ono ya kwamba siku za watu wake zilikuwa zimekwisha, na kwa wakati fulani, naye aliwaona Mataifa wakiingia. Kisha akaona ono la hili jiwe kubwa mno hapa, ama sanamu hii kubwa mno, iliyokuwa na kichwa cha dhahabu, na kifua cha fedha. Sasa angalia, inazidi kuwa ngumu, kutoka fedha mpaka dhahabu. Nyingine, mapaja ya chuma . . . ama mapaja ya shaba. Halafu miguu na nyayo za chuma. Lakini vidole vya miguu, vilikuwa kumi, na vidole hivyo vya miguu vilikuwa vya chuma na udongo. Naye akasema, "Kama vile ulivyoona ya kwamba chuma hakingechanganyika na udongo, falme hizi zilizogawanyika hazitachangamana mmoja kwa mwingine, lakini zitajichanganya mbegu zao pamoja, zikijaribu kuvunjana nguvu zao." Mnaona?

121 Sasa, jambo ni kwamba, kile kichwa cha dhahabu kilikuwa ni Nebukadreza, jinsi alivyoifasiri. Kasema, "Mfalme mwingine atakuja na atakuwa mdogo kuliko wewe," ambaye alikuwa ni Dario, yule wa Wamedi na Waajemi, akichukua mamlaka juu ya ufalme wa Mataifa. Huo mwingine ulioingia, baada ya Wamedi na Waajemi, ulikuwa upi? Wayunani, yule Aleksanda Mkuu, na kadhalika; Wayunani walitwaa mamlaka juu ya huo ufalme. Halafu ni akina nani walioutwaa kutoka kwa Wayunani? Warumi. Na ni nani wameutawala ulimwengu wa Mataifa tangu wakati huo? Warumi! Warumi, sasa, huo ulikuwa chuma.

122 Halafu angalia, Rumi inadumu mpaka mwisho, kwa sababu ilifikia kwenye mwisho wa vidole. Naye aliona matope, udongo; na hao ni watu, kitu tulichoumbwa kwacho. Na chuma, zile nguvu za Rumi, zinaenea katika kila moja ya mataifa hayo. Na Rumi ina nguvu katika kila taifa chini ya Mbingu.

123 Kuna mtu mmoja duniani anayeweza kusimamisha vita ama kuanzisha vita, bila ninii . . . kwa kusema neno moja. Huyo ni papa. Vipi kama angalisema, "Mkatoliki ye yote asiingie vitani." Hilo linatosha, ndugu, sema lo lote utakalo. Sehemu kubwa ya ulimwengu, ya Kikristo, ni Katoliki. Mnaona? Vema. Hebu aseme neno moja, ndilo hilo hilo tu.

124 Ni kama tu vile walivyosema hapa, "Nani . . . " Tutaliingilia baadaye. "Ni nani awezaye kufanya vita na huyo mnyama? Ni nani awezaye kunena kama yeye? Ni nani awezaye kufanya jambo hilo? Basi, na tufanye sanamu mfano wa huyo mnyama." Huo ni muungano wa makanisa, "tufanye sanamu mfano wake." Mnaona? Kuyaunganisha madhehebu pamoja, jambo ambalo

wamelifanya tayari. Loo, tuko mwisho tu. Hakuna lingine, rafiki. Tuko hapa mwishoni. Unaona? "Na tufanye sanamu ya mnyama," kitu fulani kama yeye. Sanamu ni kitu fulani kinachofanana na kitu kingine. Unaona? Sasa tuko wakati wa mwisho.

125 Sasa angalia hapa, katika mwisho wa wakati huu. Sasa, Danieli, katika mlango wa 2, na kifungu—kifungu cha 34 na 35, yeye aliiangalia sanamu hii akastaajabu ajabu kuu. Naye aliiangalia mpaka jiwe likachongwa mlimani, bila kazi ya mikono, nalo likafingirika likaipiga ile sanamu kwenye miguu yake, likaivunja hiyo. Basi, halikuipiga kichwani, sasa. Liliipiga miguuni; hiyo ilikuwa ni katika mwisho wa wakati, hivyo vidole kumi vya miguu.

126 Je! ulichunguza, ndivyo ilivyo kabisa, kabla tu Bw. Eisenhower hajatoka, yule Mprotestanti wa mwisho wa... wa Marekani, katika—katika Rais, jambo ambalo nina shaka kutawahi kuwa na mwingine. Lakini—lakini wakati...ili kuonyesha tu ya kwamba, laiti watu wangaliamka. Wakati alipokutana, walikuweko...Ule mkutano wa mwisho ambao (wao) yeye aliufanya pamoja na Urusi, kulikuweko na nchi tano za kikomunisti za Mashariki zilizowakilishwa, nchi tano za Magharibi. Bw. Khrushchev alikuwa ndiye kiongozi wa nchi za Mashariki. Bw. Eisenhower alikuwa kiongozi wa nchi za Magharibi. Na Khrushchev, ninavyofahamu na nilivyoambiwa, ya kwamba katika lugha ya Kirusi, *Khrushchev* maana yake ni "udongo." Na *Eisenhower* maana yake ni "chuma," katika Kiingereza. Hicho hapo chuma chenu na udongo, havitashikamana. Naye alivua kiatu chake na kupiga meza nacho, na kila kitu. Havitashikamana.

127 Lakini ilikuwa ni katika siku za dola hizi ambapo ule Mwamba, Jiwe lililokatwa mlimani, bila kazi ya mikono, lilipoipiga ile sanamu miguuni mwake. Sasa, "Kukatwa kutoka kwenye mlima." Hapana budi ulikuwa ni mlima wa mawe. Lilichongwa kutoka kwenye mlima wa mawe. Sasa, uliona?

128 Sasa, ndugu zangu wahudumu, na ndugu na dada, kila mahali ulimwenguni. Ninavyofahamu mimi, Biblia ya kwanza iliyoandikwa, Mungu aliiandikia mbinguni, maana hawana budi kuangalia juu na kuona ya kwamba kuna Mu—Mungu Mbinguni, ya kwamba Mungu yuko juu yao. Na kama ukiangalia katika Zodiaka... Sasa hata mmoja wenu asiende...Ninyi dumuni papa hapa na Biblia. Mnaona? Lakini, ile—ile Zodiaka inayoninii, inayoanza kwanza katika Zodiaka, ninavyofahamu, ni bikira; wa mwisho katika namba ya Zodiaka ni Leo yule Simba. Huko ni kule Kuja mara ya kwanza kwa Kristo, kupitia kwa bikira; kule Kuja kwa pili, ni Simba wa kabila la Yuda. Unaona? Halafu tunapata wakati wa kaa, na, pia, kushuka katika zodiaka.

129 Sasa, tunaona ya kwamba kulikuwa na nyingine iliyoandikwa, ama nyingine iliyowekwa, na hiyo ilikuwa ni zile piramidi. Ulipata kuona katika zile piramidi, jinsi ilivyoanza, ikiwa ni pana chini, kama mlima, ulioumbwa kwa mwamba mtupu, ikapanda moja kwa moja hata ikafikia juu kabisa? Lakini hapajakuwepo kamwe na kifuniko kilichowekwa juu ya ile piramidi, ile piramidi kubwa kule Misri. Chukua ninii yako. . . Kama una noti ya dola moja mfukoni mwako, chukua noti ya dola na uiangalie. Nawe utaona hapa ule Muhuri wa Marekani upande mmoja, na upande huo mwingine ina ninii, chini yake, piramidi. Na juu ya piramidi, lile jiwe la kufunika, lakini ni jicho kubwa. Na inaitwa, hapa chini ya piramidi hii, "Ule muhuri mkuu." Kwa nini tai wa Marekani siye ule muhuri mkuu? Huo ni muhuri wa Mungu. Kumbukeni, tulikuwa tukiimba wimbo mdogo:

Kote kote barabarani mpaka kwenye makao ya
  kweli ya nafsi,
Kuna Jicho linalokuangalia;
Kila hatua unayopiga, Jicho hili kuu liko
  macho,
Kuna Jicho linalokuangalia.

Hiyo ni kweli. Kumbukeni, tulikuwa na yubile ndo—ndogo, tunasema.

Kama ukiiba na kudanganya na kuhadaa, na
  kanisani unashuhudia,
Kuna Jicho linalokuangalia.

130 Sasa, ule muhuri mkuu. Sasa, tunajua, nami sifahamu jambo hilo, kule kuipima ile piramidi. Lakini nimekuwa nikiwaambia ninyi watu katika ninii ya mwisho, katika baadhi ya mafundisho haya yanayokuja, ili mpate kuona yote yanaendelea mbele tu, kwa pamoja.

131 Sasa, piramidi ilianza, kuliwakilisha Kanisa, ni pana upande wa chini. Na wakati inapokaribia kilele, inaanza kuchukua zaidi na zaidi umbo la—la mpare.

132 Sasa, tunaona, inafikia moja kwa moja hadi kileleni kule juu wala wao hawajawahi kamwe kuimalizia. Kwa nini? Kwa nini? Nashangaa ni kwa nini! Kwa sababu Biblia ilisema Jiwe la Kuweka Juu lilikataliwa. Hayo yalikataliwa.

133 Sasa angalia, wakati wa kanisa. . . Sikilizeni kwa makini sasa. Msikose jambo hili. Wakati wa kanisa umekuja kutoka mwanzo wa yale matengenezo, Luther, ukirudi nyuma katika nyakati zile ambapo mawe ya msingi yaliwekwa, ambayo ni mafundisho ya mitume. Ndipo tunaona, wakati ulipoendelea, kutoka wakati mmoja kuingia mwingine, Kanisa liliendelea kuwa katika uchache wakati wote. Mpaka, lilipitia kama. . . Luther alihubiri kuhesabiwa haki. Halafu, kuninii tu, kukikiri

tu ya kwamba wewe ni Mkristo, wangekuua, zile siku za ufia imani, wafia imani.

134 Basi tunaona, katika siku za Wesley, ulikuwa mtakatifu anayejifingirisha kama ulimkiri Kristo wakati huo, huyo Mmethodisti mpya. Watu walitoka hapa nje wakati Wesley alipokuja hapa, na Asbury, walikuwa na mikutano hapa Marekani, tukisoma historia yao, ambapo waliifanyia katika nyumba za shule. Makanisa yao hapa hayangewaruhusu. Na hatimaye wakafikia mahali hata Roho Mtakatifu angewashukia, nao wangeanguka sakafuni, na wangewamwagia maji, wakawapepea kwa kipepeo, wakifikiri walikuwa wamezimia. Nami nimehudhuria mikutano yao mimi mwenyewe, katika miaka yangu ya hamsini. Na nimewaona wakianguka chini ya nguvu za Roho Mtakatifu namna hiyo, na wangewatupia maji usoni mwao, na kila kitu, wale Wamethodisti huru wa zamani, miaka mingi iliyopita. Hicho kilikuwa ni kipindi cha mateso.

135 Sasa, basi, baada ya wakati huo kwisha, huo wakati wa Kiwesley, ukaja wakati wa Kipentekoste pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnaona, linaumbika, wakati wote. Sasa kumbukeni, hilo Jiwe la Kuweka Juu bado halikuwa juu yake. [Ndugu Branham aliandika jambo fulani ubaoni na kuligotagota kwa chaki mara mbili—Mh.] Kwa nini? Wao walilijenga Kanisa vile ilivyopaswa hasa, ama walilijenga piramidi katika umbo la kuungana na Jiwe la Juu, lakini hilo Jiwe la Kuweka Juu halikuja kamwe. Loo, mnaona mahali nilipo, sivyo!

136 Sasa, ile huduma kutoka kwa Luther hata mwisho wa Pentekoste, katika lile kundi dogo sana hapa juu. . . Hiyo ndiyo sababu Mwanga ulikuwa karibu kutoweka, katika wakati huu, pale kwenye ile kalenda, kwenye ile jedwali. Ni wakati wa kipentekoste, wa kipentekoste; si—si madhehebu ya Kipentekoste, maana wao walifanya vile vile kabisa kama Walaodikia. Wao ni Walaodikia. Walifanya kama Wanikolai, wakaunda madhehebu.

Lakini Kanisa la kweli, kila mahali ulimwenguni, limejengwa kufikia mahali ambapo kumekuja huduma katikati Yake, ilinganayo na huduma ya Yesu Kristo kabisa. Sasa wao wana nini? Wamekitayarisha kitu hicho. Sasa jambo linalofuata ni nini? Hili Jiwe lililokataliwa, la piramidi, lilikatwa mlimani (bila nini?) kazi ya mikono. Mungu alilituma. Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yule aliyekataliwa, lile Jiwe lililokataliwa, ndilo kichwa cha Hili; ndilo kichwa, lile jiwe la kifuniko. Na yule yule waliyemkataa, katika wakati mzima wa Mataifa, ni Kristo. Naye Kristo hakukatwa na kuwekwa hapa ndani kama halifa, ama mwana mdogo wa Mungu, ama mheshimiwa fulani mkuu kanisani. Yeye ni Roho Mtakatifu. Na kile kifuniko cha piramidi kitakuwa ni Kristo akija. Mnaona jambo hilo? [“Amina.”]

137 Sasa, kwa sababu ya kwamba wao wako katika umbo, (Mnaona mahali ambapo nimelifanyiza hili kama piramidi, kule kufufuka kwa watakatifu?) kunafanya safari ya kwenda kuingia Utukufuni. Mnalipata jambo hilo sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kristo, lile Jiwe la Kuweka Juu, Jiwe lililokataliwa, lile Jicho lionalo yote, akija kulingana kabisa na Biblia ilivyosema. Naye Danieli alisema aliuangalia wakati huu wa Mataifa mpaka Jiwe likatoka mlimani, ambalo halikuchongwa kwa mikono. Wao hawajaweka wakati wo wote jiwe la kufunika kwenye hiyo piramidi. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara mbili.] Halikuchongwa na mikono ya binadamu. Mkono wa Mungu ndio uliolikata Jiwe hilo. Mnaliona? ["Amina."] Nalo lilifanya nini? Liliipiga sanamu ile moja kwa moja miguuni, na kuivunja vipande-vipande, na kuisaga kuwa kama unga. Haleluya! Ni jambo gani lililotukia wakati huo, kule kuja kwa hilo Jiwe? [Ndugu Branham anapiga mimbara mara nne.] Kanisa likapaa Juu Utukufuni, katika kule Kunyakuliwa, maana lilimalizia kile kipindi cha Mataifa. Mungu alikimalizia; kule kuja kwa lile Jiwe.

138 Kulikuwa na watu waliokuwa wakija hapa kanisani, maskini mwanamume mmoja na mkewe. Wangeichukua Biblia na kuiweka chini mahali fulani; nao wangeenda, wakiimba:

> Loo, ninalitafuta lile Jiwe lililokuwa likifingirika huko Babeli,
> Likifingirika huko Babeli... (Wakizunguka, wakilitafuta hilo, mnaona.)
> Ninalitafuta hilo Jiwe lililofingirika likaingia Babeli.

139 Huyo hapo! Kristo ndiye hilo Jiwe. Yeye hakuzaliwa na mwanadamu. Alizaliwa na Mungu. Yeye anakuja kwa ajili ya Kanisa ambalo limezaliwa mara ya pili, kwa Roho wa Mungu, maana nguvu za Jiwe hilo la Kuweka Juu zinapitia kote kote Kanisani, kama sumaku.

140 Ninakumbuka kuhusu nilipokuwepo hapa, nikiangalia ule mtambo wakati ule, mahali walipokuwa wakiunda vitu hivyo vyote. Na takataka hizo zote zilizokuwa pale, nao wakazifagia. Hilo jiwe kubwa lilikuja likaziokota, hiyo sumaku kubwa ya jiwe, na kuziokota zote kwa sababu zilishikwa na sumaku ya lile Jiwe.

Hatuna budi kutiwa sumaku inayokamatwa na hilo Jiwe la Kuweka Juu. Hilo Jiwe la Kuweka Juu ni Roho Mtakatifu, Kristo. Na kila mmoja wetu ana sumaku hiyo ya Roho Mtakatifu. Wakati lile Jiwe litakapoipiga ile sanamu, Kanisa litakimbilia Kwake, lirudi Utukufuni. Litanyakuliwa, katika kule Kunyakuliwa kwa watakatifu, wakati litakpoondoka katika siku ile.

141 Sasa, angalieni hapa. Tunaona ya kwamba, Wayahudi wamekuwa sasa wakirudi, kwa kama miaka arobaini, karibu wakati ule ule uliotumika kufikia yale maangamizi ya hekalu. Imewachukua kama miaka arobaini kurudi, mpaka kule kujengwa upya kwa hekalu lingine. Unaona, tuko kabisa mwisho wa safari. Vema, kama Mataifa . . .

142 Sasa hebu na tuchukue ninii . . . Tunaliona Kanisa, kule kuja kwa lile Jiwe. Hebu tuchukue wakati wa mwisho. Tulipitia jambo hilo. Tunaona sasa. Ninaamini nina maandishi hapa juu ya jambo hilo. Hebu tuone, hebu kidogo. "Na yule aliye mkuu anayekuja, ambaye ni mpinga-Kristo, atafanya agano na Wayahudi." Na katika Danieli mlango wa 7 . . . ama—ama 9:27. "Na katikati ya lile juma, ile miaka mitatu na nusu, yule mnyama atafanya agano lake . . . " Ni—ninataka kufikia jambo hilo, baadaye kidogo, lile agano. Tunataka kuondoka . . . Ninataka kuanza papa hapa sasa.

143 Kila mmoja wa nyakati hizi za Mataifa zimethibitishwa bila kukosewa kuhusu mjumbe wao, ujumbe wao, na mambo ambayo yangetukia.

Wakati *huu* hapa ulikuwa ni wakati wa fahari sana.

Wakati uliofuata, ilisema kungekuweko na fundisho linaloitwa, ama kitu fulani kilichokuja, kinachoitwa "mi— misemo ya Wanikolai."

Ndipo ikafikia, jambo la pili, linakuwa fundisho.

Ndipo kukaja, ndoa ya ninii . . . kwa kanisa la Wanikolai, na mateso ya watakatifu. Kila kitu kilitukia namna ile ile tu.

Tunafikia kwenye jambo hilo lingine, Nuru kidogo tu ilianza. Una nguvu kidogo, na una jina ambalo unaishi, bali umekufa. Tia nguvu hicho ulicho nacho tayari, nisije nikaja, nikaondoa kinara cha taa."

144 Ndipo akaja Wesley, baada ya wakati huo, pamoja na wakati wake. Tuliona vile vile hasa kile . . . Wakati wa Wesley, uliitwaje? Wa Filadelfia. Wakati mkuu sana wa—wa upendo tuliopata kuwa nao, wakati wa Filadelfia, ulikuwa hasa katika wakati wa John Wesley.

Wakati alipotoka, wakaingia Wapentekoste, na hao walikuwa vuguvugu.

Kisha tunarudi na kuona ni Ujumbe wa namna gani ungekuja kwa Wapentekoste, wakati wa mwisho.

Kumbukeni, kila mmoja alikuja mwishoni mwa wakati huo wao. Mtakatifu Paulo alikuja mwishoni. Hao wengine walikuja mwishoni, Mtakatifu Ireneo na hao wengine wote. Wakati wa huyo mwingine uliendelea hata kwenye huo mwingine, zikapitana, naye akauchukua na kuenda kwenye wakati huo mwingine nao. Mnaona?

145 Sasa, tunaona, katika wakati huu, kuna nyota, kama tuliyo nayo pale. Tuna nyota, mjumbe. Tuna mtu, U—Ujumbe unaotangazwa kwa wakati huu; watu wa kuukataa Huo; watu wa kuupokea Huo. Na mjumbe wa wakati huu alikuwa aje katika nguvu za Eliya. Hiyo ni kweli. Naye alikuwa "Airudishe imani ya watoto iwaelekee baba zao, kuwarudisha masalia ya pentekoste, waliosalia, wairudie Imani ya kweli ya kimitume."

146 Sasa, Imani ya kweli ya kimitume, kama utasoma katika Kitabu cha Matendo ya Mitume, utaona ya kwamba hapajawahi kamwe kuwepo na wakati hata mmoja mtu aliyewahi kubatizwa, "jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.'" Hakuna hata mmoja wao aliyewahi kunyunyiziwa. Hapakuwepo na upuuzi wo wote kama huu tulio nao unaoendelea siku hizi, unaoitwa Pentekoste, uliowahi kutukia kule nyuma. Wao walikuwa na madhihirisho ya kweli, na Roho wa Mungu akiwa miongoni mwao, aliyekuwa Mwana wa Mungu asiyekosea akitenda kazi miongoni mwao.

Mtu huyu ambaye alikuwa aje, Ujumbe huu, hasa, ambao ulikuwa uje, ulikuwa uwe kama Eliya. Eliya alikuwa aje mara tatu.

Sasa mnasema, ya kwamba, "Yohana Mbatizaji alikuwa ndiye jamaa huyo." Kama ukiangalia, Yesu alisema Yohana Mbatizaji alikuwa ndiye mjumbe wa Malaki 3, si Malaki 4. "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu." Nafikiri Mathayo 11:6, moja kwa moja mahali hapo utapata jambo hilo, Mathayo sura ya 11.

147 Sasa, lakini katika siku hizi za mwisho, itakuja Roho ya Eliya miongoni mwa watu, naye atafanya jambo lile lile ambalo walifanya kule nyuma. Tabia yake ingekuwa ni kitu kile kile, tabia ya Kanisa. Tabia ya m—mtu huyo ingekuwa ni ile ile hasa. Na ujumbe huo unaotoka, kujaribu . . . Yeye angechukiwa, na watu. Angewachukia wanawake, walio wazinzi, hata hivyo, walio wabaya. Atapenda nyika; atakuwa ni mtu wa huzuni, mwenye wasiwasi wakati wote, kama alivyokuwa Eliya, na kama alivyokuwa Yohana Mbatizaji. Nasi tumeona mambo haya yote yakitimia. Kama tumekuwa na Ujumbe, tunamwona Kristo akikataliwa. Huna budi kuwa mfuasi wa moja ya madhehebu haya la sivyo huwezi kuingia ndani yao. Kwa hiyo, Yeye, Yeye ametupwa nje. Unaona? Kristo hawezi kutenda kazi miongoni mwao.

"Wewe ni nani?"

"Mkristo."

"Wewe ni wa madhehebu gani?"

"Sina yo yote."

"Hatuwezi kukutumia."

148 Unaona, Yeye amekataliwa. Kweli! Unaona, amekataliwa! Vivyo hivyo Eliya naye alikataliwa, na vivyo hivyo Yohana

alikataliwa. Lakini, nini, liliwaudhi? Lilidhuru ujumbe wao? Wao walisema, "Loo, enyi wenye shingo ngumu." Waliwakemea. Hawakuwachezea. Waliendelea moja kwa moja. Nao Ujumbe wa Mungu utaendelea moja kwa moja, haidhuru mtu ye yote aliyosema nini, unaona, mpaka mwisho, na wakati ninii . . . yale yaliyokusudiwa yatakapomwagwa. Nasi tuko mwisho.

149 Basi, tunajikuta wenyewe sasa, katika miaka arobaini ya kurudi, tangu Vita vya Kwanza vya Dunia, na Wayahudi wamerudi kwenye nchi yao. Mungu kamwe hakuwashughulikia Israeli mpaka walipokuwa katika nchi yao wenyewe.

150 Sasa, mnakumbuka wakati Wayahudi walipokuwa wanarudi, hao Wayahudi kutoka huko katika mataifa mengine, na gazeti la *Look* likatoa makala yake. Nilisoma kisehemu kilichokatwa kutoka kwenye gazeti fulani, gazeti fulani la kidini, ya kwamba wakati wao . . . Hizo ndege ziliposhuka kwenda kule kuwachukua hawa Wayahudi huko mbali Iran. Nami sijui walikokuwa hao wote, walitawanyika tu kule.

Sasa, hao ndio Wayahudi wa kweli, hao ambao hawakupata kuwa na nafasi. Sasa, ndugu, hao hapo wale mia na arobaini na nne elfu wako. Tutakapofikia Ufunuo 11, utawaona. Yeye alisema, "Kuna makabila kumi na mawili (ya Gadi), makabila kumi na mawili (ya Asheri), makabila kumi na mawili (ya Reubeni), makabila kumi na mawili . . . " Na hao wote walikuwa wakisimama wapi? Juu ya Mlima Sinai. Wayahudi, wamerudi katika nchi ya uenyeji wao, walikuwa ndio hao hapo. Ndio hao ambao hawakuwa kundi hili la wahuni wa Wall Street. La, bwana. Walikuwa ni wale Wayahudi halisi.

151 Na wakati maskini rabi huyu mzee aliposimama kule nje na kuona ndege hii ikitua, hao Wayahudi. Mlisoma jambo hilo kwenye gazeti. Walikuwa wangali wakilima kwa plau zao za miti. Na basi walipoona kitu hicho kimetua kule nje, hawakuwa wakipiga kona. Yule rabi mzee alisimama pale akasema, "Kumbukeni, nabii wetu alisema, 'tutakaporudi katika nchi ya uenyeji wetu, tutabebwa kwenye mbawa za tai.'"

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara walizotabiri manabii.

Hata tunajiandaa kufikia juma hilo la saba kwa ajili yao.

152 Nafikiri, mimi mwenyewe, nikiwa nimesimama kule nje, wakati Ndugu Pethrus alipowapelekea hizo Agano ndogo, nao wakazisoma. Wakasema, "Vema, kama huyu ndiye Masihi, hebu—hebu na tumwone Yeye akifanya ishara ya Nabii, kama Yeye hajafa, Yeye yu hai." Wakasema, "Yeye alifufuka tena; anaishi katika Kanisa Lake; hebu na tumwone akifanya ishara ya Nabii, nasi tutamwamini." Wayahudi daima wanaamini . . . Wanajua Masihi alikuwa awe Nabii.

153 Na wakati niliposimama kule ng'ambo kwa Ndugu Arganbright siku ile, mahali pale, na hao Wayahudi wakiwa

wamesimama pale, wakasema, “Hebu njoo tu kwetu, kwa watu wetu.”

154 Nikasema, “Hakika, nitafurahia kuja.” Nikatoa tu uamuzi, upesi kupita kiasi.

155 Nikafika Cairo, Misri. Hivi majuzi usiku, nilipoona hiyo ndege ikishuka kule Cairo, ilinikumbusha. Kwa hiyo wakati tuliporudi kule, nami nilikuwa na tikiti yangu ya kwenda Israeli, walikuwa waje kunilaki. Nikasema, “Nenda, kawakusanye maelfu wachache wa hao viongozi. Waleteni huko kwenye ndege mahali fulani, tutaona kama Yeye angali ni Nabii ama si nabii. Amina. Vema, hebu tuone atakalofanya.” Loo, hilo lilikuwa tu moja kwa moja mkononi mwao. Hicho ndicho walichotaka. Kama wangeweza kuona jambo hilo, wangeamini.

156 Kwa hiyo nilifanya nini? Nikaenda kule Cairo, kisha nikaanza kupanda. Tayari nilikuwa na tikiti yangu; karibu dakika ishirini kufikia wakati wa kuitwa. Kitu fulani kikasema, “Si sasa. Kikombe cha maasi ya Mataifa, hakijajaa bado. Cha waamori hakijatimia. Usiende huko!” Nilifikiria labda mimi niliwazia tu jambo hilo, na nikaenda nyuma ya lile banda la eropleni na kuomba. Kasema, “Usiende huko sasa.” Ndipo nikaitwaa tikiti yangu nikaenda mahali pengine. Sikwenda, kwa maana wakati haujawadia bado.

157 Sasa, ni wakati gani ambao Mungu atawaruhusu hao Wayahudi, kuanza kushughulika nao tena, sijui. Sijui. Hakuna anayejua jambo hilo. Lakini, sikilizeni, kama Israeli tayari wako kwenye nchi ya uenyeji wao, mambo yako tayari kabisa. Mawe yote yameokotwa, na umwagiliaji, yale maji, na kila kitu alichoahidi Mungu. Wamepata visima vya mafuta na kadhalika, na mito mikubwa iliyo wazi, hapo ndipo mahali pazuri sana ulipopata kuona. Wamejenga mji kule. Wana umwagiliaji. Wana ardhi iliyo nzuri kuliko ardhi yo yote ulimwenguni, kule. Nasi tunaona, mumo humo katika Bahari ya Chumvi, mna kemikali nyingi zaidi, za kutosha, kuununua ulimwengu mzima. Mnaona?

158 Kila kitu kimeangukia moja kwa moja mikononi mwao. Walifanya jambo hilo namna gani? Kwa sababu moyo wa Hitler ulifanywa mgumu, moyo wa Musolini ulifanywa mgumu, kama tu vile moyo wa Farao ulivyofanywa mgumu, na kuwarudisha kwenye nchi hiyo. Na kwa miaka arobaini wamekuwa wakirudi kwenye nchi hiyo. Sasa ndio hao humo wameketi, wanangoja.

159 Kanisa la Mataifa liko katika Laodikia, mwisho wa Wakati wa Laodikia. Kama . . . Wayahudi wako kwenye nchi ya uenyeji wao, wako kule tayari. Na ukengeufu wa Mataifa tayari umetukia. Na tuna rais kama tuliye naye. Tuna taifa lililofilisika kama tulilo nalo. Tuna mabomu ya atomiki yakining’inia kwenye mabanda. Tuna kanisa lililo vuguvugu. Tuna Kanisa, watu, waliokusanyika pamoja. Tuna huduma ambayo inalingana na huduma ya Yesu Kristo, kuungana na lile Jiwe litakapokuja.

Ni kitu gani kimesalia? Inaweza kuwa dakika yo yote. Hakuna kitu kingine kilichosalia. Tuko katika wakati wa mwisho. Loo, utukufu! Sijui kama nitaweza kamwe kuwa katika yubile hiyo, ama sitakuwa, lakini ninataka tu—ninataka tu kuwapa sehemu yake, hata hivyo.

160 Sikilizeni. Je! . . . Ni wangapi wanaoweza kuona sasa? Mnaona ambapo Maandiko huthibitisha ya kwamba yale majuma sabini yalikuwa miaka arobaini na tisa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona ambapo yale majuma sitini na mawili yalikuwa ni miaka mia nne na thelathini na minne? ["Amina."] Mnaona mahali ambapo yale—yale majuma sitini na tisa basi ya—ya—yalikuwa . . . Ilikuwa ni kitu gani? mia nane na . . . Miaka mia nne na—na themanini na mitatu. Miaka mia nne na themanini na mitatu hadi wakati huu. Mnaona mahali yule Mkuu alipokatiliwa mbali? Mnaona, mnachukua miaka arobaini kwa hao Wayahudi hatimaye kuingia mahali pao, ambapo Mungu alisema.

161 Angalia hapa ambapo wakati wa Mataifa umepitia kila kitu tulichosema ungekipitia; ambapo, si kwamba *sisi* tulisema ungefanya hivyo; yale Biblia ilisema wakati huo ungepitia. Yale Biblia iliyosema wakati wa Mataifa ungefanya, kuja moja kwa moja hadi wakati huu wa mwisho; na kwa miaka arobaini hao Wayahudi wamekuwa wakirudi humu, wakijiandaa kusudi Mungu afanye yale hasa aliyofanya hapa. Walitoka namna hiyo, na wakaingia namna hiyo. Nayo Israeli imerudi katika nchi ya uenyeji wake.

162 Sasa, Mungu ataanza juma lao la mwisho lini? Lini? Huenda ikawa ni leo. Huenda ikawa ni kabla ya jua halijatua usiku wa leo. Mungu atatangaza jambo hilo. Kwamba ni wakati gani, mimi sijui. Ninashangaa. Lakini nitaleta jambo fulani hapa, sasa, katika dakika chache, wala sijui kama mtaliamini ama hamtaliamini. Lakini si—si—sina budi kulisema, hata hivyo, ninaamini.

163 Tuko katika nchi ya uenyeji wetu. Wayahudi wako katika nchi ya uenyeji. Tuko katika mwisho wa wakati, tayari kwa Kunyakuliwa. Kunyakuliwa kunakuja, Kanisa linapaa juu, tunanyakuliwa kumlaki Yeye hewani. Sote tunajua jambo hilo. Lile Jiwe lililokatwa mlimani, liko tayari kuja wakati wo wote. Na hapo litakapokuja, litafanya nini? Linaishiliza wakati wa Mataifa. Umekwisha, Naye Mungu anaacha kabisa kuwashughulikia. "Mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; mtakatifu na azidi kutakaswa." Mnaona? Yeye anafanya nini basi? Analichukua kanisa Lake, lililojawa na Roho Mtakatifu.

164 "Uchafu" ni nini? Hao ni wanawali waliolala na hao wanaokuja hukumuni, mbali sana *huku*. Tutapata jambo hilo kwenye ramani nyingine, tutakapoendelea na jambo hili hapa, ambapo wanakuja kwenye kile Kiti cha Enzi Cheupe cha

Hukumu na hawana budi kuhukumiwa na waliokombolewa. Paulo alitwambia tusipeleke daawa kortini, kwa sababu watakatifu wataihukumu dunia. Hiyo ni kweli. Tuko katika wakati wa mwisho, *hapa*, sasa. [Ndugu Branham anarejea kwenye mchoro wake ubaoni—mh.] Vema.

165 Na katikati ya juma hili . . . Sasa, haya hapa yale sabini. Sasa, kama hii ilikuwa miaka saba kamili, kila moja ya majuma hayo, na tayari tumeshakuwa na majuma sitini na tisa; basi tuna wakati wa Mataifa, nasi tunajua ya kwamba tuko katika mwisho wa wakati wa Mataifa; ndipo kuna juma moja zaidi lililosalia kwa ajili ya Wayahudi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Na hilo ni miaka saba kamili. Kama *hii* ilikuwa ni miaka saba, *ile* ni miaka saba, maana Yeye alisema, "Majuma sabini yameamriwa juu ya watu wako." Kwa hiyo tunajua tuna miaka saba kwa ajili ya Wayahudi. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Sasa angalia jambo hilo. Kama kuna swali, ninataka kulijua. Mnaona?

166 Sasa, na katikati ya lile juma, katikati ya juma hili la Wayahudi; mnaona, hiyo ni miaka—miaka mitatu na nusu; mpinga-Kristo, yule mkuu, mkuu atakayekuja. Pia kumbukeni, yeye anatokea Rumi, yule mkuu atakayekuja. Yeye ni nani? Papa. Mkuu miongoni mwa watu, atakayekuja, atainuka Farao asiyemjua Yusufu.

167 Sasa, ninyi Waprotestanti mnasema, "Vema, sasa, jambo ndilo hilo." Lakini hebu kidogo. Tunaona ya kwamba Waprotestanti wana madhehebu, wanafanya muungano wa makanisa, sanamu ya mnyama, na wanaambatana moja kwa moja pamoja nao.

168 Nasi tunaona hapa ya kwamba Wayahudi wanaitwa katika muungano huu, (naam, bwana), nao wanakubali. Na Biblia ilisema ya kwamba walikubali. Naye anafanya agano nao.

Hapo katikati ya juma la sabini likiendelea, yeye anavunja, mpinga-Kristo anavunja agano lake na Wayahudi, "watu wako." Kwa nini?

Na tunasoma katika Ufunuo 11, ya kwamba, "Nitawatuma . . . " Hiyo ni 11. Unakuja kukaribia 19 sasa. Ya kwamba atawatuma manabii Wake wawili, nao watatabiri katika wakati huo, ndipo watakasirishwa na manabii hawa na kwa kweli watawaua. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na maiti zao zitalala kwenye barabara ya kiroho inayoitwa Sodoma na Gomora, ambapo Bwana wetu alisulibishwa, Yerusalemu. Hiyo ni kweli?" ["Amina."] Nazo zikalala pale siku tatu mchana na usiku. Na baada ya siku tatu usiku na mchana, roho wa uhai ataingia ndani yao, nao watafufuka na kuingia Utukufuni. Sehemu ya kumi ya mji ilianguka wakati huo. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Mnaona? Ni kitu gani hicho? Katikati ya miaka hii sabini ya mwisho.

169 Wakati Kanisa litakaponyakuliwa; ndipo ule muungano, mwanamwali aliyelala. Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbiteri, na Mpentekoste vuguvugu, wote hao pamoja kwenye muungano. Ambapo, tayari wamepata utawala wao mkubwa sasa. Na wanapofanya jambo hilo, watafaya agano. Na, vema, sasa, papa huyu mpya tuliye naye sasa anataka kuwaingiza wote ndani. Je! hamwezi kuona jambo hilo likifura? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nitazungumza juu ya jambo hilo, na kuwaingiza wote ndani, mara ya kwanza kwa mamia na mamia na mamia ya miaka; miaka elfu moja, ama mbili, limewahi kutendeka. Lakini sasa Yeye hana budi kuwaingiza wote ndani, pamoja, na kufanya muungano, na humo ndani Wayahudi watakubali jambo hilo. Loo, jamani! Utukufu! Haleluya! Mungu wetu na asifiwe aliye hai milele na milele! Haya basi! Sasa, ndugu, ni rahisi tu, rahisi kama vile mtoto mdogo angaliweza kuliona. Ule muungano wa kuwaleta Wayahudi, na Waprotestanti na Wakatoliki, pamoja.

Na, kumbukeni, hawa manabii wawili watafanya nini watakapokuja?

170 Mnyama huyu, mkuu huyu atakayetawanya nguvu za hao watu watakatifu, yeye atafanya nini? Atavunja agano lake nao. Baada ya miaka mitatu na nusu, atawaondosha. Sasa, watu wanafikiri huo ni ukomunisti. Hiyo ni kwa sababu tu ninyi . . . Roho wa Mungu hajawashughulikia bado. Si ukomunisti; ni dini. Biblia ilisema, "Watafanana sana hata jambo hilo lingewadanganya walio Wateule kama yamkini." Yesu alisema hivyo. Mnaona, tuko kwenye la mwisho.

171 Sasa, hawa manabii wawili, watafanya nini? Ni Musa na Eliya watakaosimama uwanjani. Watawaambia hao Wayahudi kosa lao. Na kutoka kwenye kundi hilo la Kiyahudi lililoko kule sasa, litakalofanyiza wale mia na arobaini na nne elfu, Mungu ataita hao kwa njia ya hawa manabii. Ni kitu gani? Roho ya Eliya, itakapotoka kwenye hili kanisa la Mmataifa, itaendelea tu moja kwa moja katika Kanisa hilo la Kiyahudi, iingie moja kwa moja na kuwaita; Musa akiwepo pamoja naye. Haleluya! Mnaona jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naye atahubiri ujumbe ule ule wa pentekoste, kwa hao Wayahudi, kwamba wao walimkataa Masihi. [Ndugu Branham anagonga mimbara mara sita.] Amina! Mnaona jambo hilo? ["Amina."] Utakuwa ni ujumbe ule ule wa kipentekoste, ambao Wayahudi hawa watahubiri moja kwa moja kwao. Nao watawachukia Wayahudi hao sana hata watawaua. Nao walichukiwa na mataifa yote. Na katikati ya juma hilo, kwa sababu walikuwa wamewainua wale mia na arobaini na nne elfu wakuu na wenye nguvu. Walikuwa na Roho Mtakatifu. Na, ndugu, nena kuhusu kufanya miujiza, waliifanya. "Walifunga mbingu, wala mvua haikunya katika siku za unabii wao; wakaipiga dunia kwa mapigo, kila walipotaka." Walileta mapigo na cho chote kile. Watawapa hao Warumi shida sana. Lakini, hatimaye,

watauawa. Mungu wetu ni Mungu wa kutisha sana wakati amekasirishwa. Lakini kumbukeni, hiyo ni huko kwenye lile juma la sabini, na Kanisa liko Utukufuni, (amina), ile Karamu ya Arusi inaendelea. Naam!

172 Sasa angalia. Hapo ndipo tulipomwona akirudi kwenye lile Hekalu la ule utawala wa Miaka Elfu mahali hapa katika mwisho wa wakati wa Kiyahudi, "aliyetiwa mafuta." Huyu hapa anakuja, amepanda farasi mweupe; hao waliomfuata Yeye, juu ya farasi weupe. *Farasi*, "nguvu." Amevaa mavazi meupe; damu. . . ama vazi lililochovywa damu; ameandikwa, "Neno la Mungu." Yeye alikuja kama Mshindi mkuu, (ndiyo, bwana) kuanzisha ule Utawala wa Miaka Elfu, akaingia katika Hekalu. Utukufu! Hapo anakutana na hao mia na arobaini na nne elfu, sasa, baada ya hilo juma la sabini hapa.

173 Lile juma la sabini, jambo hili linaendelea wakati wa juma la sabini. Katika ile mitatu, katikati yake, yeye analivunja, kwa sababu yeye anawaua hao manabii wawili wa kipentekoste (. . . bwana) wanaoipiga dunia.

Na, jamani, Yeye analilaani kanisa hilo, na kuliteketeza kwa moto. Na, mbona, hilo. . . Tunaona jambo hilo pale, hata mabaharia wakisimama kwa mbali, walisema, "Ole, ole ule mji ulio mkuu wa milele wa Rumi, umefikia mwisho wake katika saa moja." Ulilipuliwa vipande-vipande. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo. Na mmoja wa Malaika akaangalia, na kusema, "Mbona, damu ya kila mfia imani wa Kristo ilionekana ndani yake," kwa ajili ya udanganyifu wake, akitoka hapa nje na kufanya madhehebu na kufanya kila namna ya upuuzi huu, na kulitia kanisa unajisi, na kuyaingiza mambo hayo mle ndani, na kuwaua wale hasa waliojaribu kulidumisha hilo na akajaribu kuwatoa nje.

174 Utukufu! Loo, si—sijui. Ni—ni—ninajisikia kama kuendelea na safari. Mnaona? Je! hamfurahi kwa ajili ya Nuru ya Mwana, kutembea katika Nuru ya Mwana! Tuko wapi, ndugu? Kwenye saa ya mwisho! Huenda jambo hilo likatukia, wakati wo wote. Tumewasili!

175 U—Ujumbe umetangazwa kwa kanisa la baadaye, kanisa lililomkataa Kristo wake. Wayahudi wako kwenye nchi ya uenyeji wao kwa kipindi fulani cha wakati, miaka arobaini. Ule mji mpya umekwisha jengwa. Wao wanatazamia nini? Masihi ajaye. Itakuwa lini? Sijui. Wakati jiwe hilo litakapoipiga sanamu hiyo *hapa*, Hilo limeondoka; yote yamekwisha wakati huo basi.

176 Sasa angalia hapa. Katikati ya lile juma, siku tatu na nusu. . . miaka mitatu na nusu, hasa, anavunja agano na kusababisha kuninii kwa sadaka na dhabihu. . . ambayo watakuwa wameianzisha tayari.

Maana, wao watarudi moja kwa moja na kusema, "Sasa, angalieni, ninyi nyote ni makanisa. Mnaweza kupokelewa katika

sanamu hii ya mnyama. Tutakuwa na ushirika. Tutaondolea mbali ukomunisti. Tutauangamiza tu ukomunisti kabisa." Mnaona? Nao wanaweza kufanya jambo hilo. Mnaona? Na watafanya jambo hilo.

177 Lakini sasa angalia. Na kuanzisha, na kuanzisha hii, ibada ya kila siku na sadaka zitarudi katika mji huo wakati hekalu limejengwa upya. Na mkuu huyu atakayekuja katikati ya juma hili, atalivunja agano lake na kukomesha zile sadaka. Lilisema, "Atazivunja, atazivunja." Na yale atakayofanya, na hilo litadumu mpaka ukomo.

178 Pia tazama:

> . . . kufanya *ukiwa*, nalo lienea hata *ukomo* . . .

"Kuenea kwa chukizo." *Chukizo* ni kitu gani? "Uchafu." Mnaona? "Kufanya ukiwa," ni kitu gani hicho? "Kuangamiza." Kuenea kwa kitu *hiki*, kuangamiza *kile*. Mnaona? Kuenea kwa hayo mamlaka ya Kirumi, kuwashinda wanawali wote wajinga, Wayahudi na kadhalika. "Sisi sote tutakuwa Warumi la sivyo hatutakuwa kitu kingine cho chote." Yeye atavunja agano lake katikati ya juma.

179 "Kuenea kwa chukizo." Kama lilikuwa ni chukizo katika wakati wa Yesu, wakati Warumi walipokuja kule na propaganda zao; itakuwa ni Rumi tena, litakuwa ni chukizo tena kwa kanisa.

> . . . kufanya *ukiwa*, na ataendelea mpaka *ukomo* . . .

Atafanya nini? Ataendelea hata ukomo, yaani, mwisho.

180 Sasa, Uyahudi, na Urumi, Uprotestanti (hiyo ni kusema, wanawali wajinga), wataungana pamoja katika namna ya muungano wa makanisa. Na itakuwa kama Yesu alivyosema katika Mathayo 24, na kutoka Ufunuo 13:14.

Hebu tufungue Ufunuo 13:14, tuone ni nini. Nilikuwa nimeliandika hapa, kuona ni jambo gani, 13:14. Vema, bwana.

> *Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya* (kuunganisha makanisa haya) *mbele ya . . . akisema . . . mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la mauti la upanga naye akaishi.*

181 Sasa, tunajua, bila shaka yo yote, huyo mnyama alikuwa ni nani, ile enzi iliyokuwa na jeraha hilo la mauti na ikaishi. Ilikuwa ni wakati Rumi ya Kipagani ilipouawa, na Rumi ya papa ikachukua mahali pake; wakati zile nguvu za kipagani zilipouawa, na nguvu za kipapa zikachukua mahali pake.

182 Sikiliza, basi, Ufunuo 13:14. Yesu, katika Mathayo 24, aliwaonya juu ya hilo. "Sanamu ya mnyama."

183 Paulo, katika Wathesalonike mlango wa 2, kifungu cha 3 na cha 4. Hebu na tulipate, unaona Paulo, kile anachosema kuhusu

hilo. Yule Roho Mtakatifu mkuu juu ya huyu nabii mkuu wa Bwana, angalia yale aliyosema juu ya jambo hilo katika siku ya mwisho. Katika Wathesalonike wa Pili, mlango wa 2 ndio huo. Vema, bwana. Na tuanzie kwenye kifungu cha 3, ninaamini ni hicho. Vema, hebu tusome sasa. Sikilizeni kwa makini, kila mtu. Ni wangapi wanaamini ya kwamba Paulo alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Angalia hapa.

> *Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote; maana siku ile haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu;. . .*

Anajaribu kuliondoa kichwani mwao ya kwamba Yeye anakuja wakati uo huo. Kasema, "Hapana budi kutokee kuanguka kutoka kwenye Kanisa, kwanza," unaona, kutokee katika Wakati huu wa Laodikia.

> *. . . .akafunuliwa yule mtu wa kuasi, ku-. . . akafunuliwa,. . .*

"Yule mtu wa kuasi," kumwasi Roho Mtakatifu. Kuasi kufunuliwe.

> *. . .mwana wa uharibifu;*

Kama alivyokuwa Yuda; mweka hazina wa kanisa.

> *Mtu yule apingaye, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa; hata yeye mwenyewe kama Mungu kuketi katika hekalu la Mungu,. . .*

Ndugu, je! kuna mtu duniani, nje ya Vatican, anayefanya jambo hilo? Liko jambo hilo?

184 Sasa, twendeni hapa katika Ufunuo 13, niwaonyeshe ya kwamba mtu huyu anakaa kwenye mji. . .katika mji fulani, na mji huo unakaa juu ya—juu ya milima saba. Na hesabu ya mnyama huyo ni mia sita sitini na sita, imeandikwa katika Ki—Kilatini. . .Alfabeti za Kirumi, ni mia sita sitini na sita, ni VICARIVS FILII DEI, ambalo ni, "Badala ya Mwana wa Mungu," kwenye kiti cha enzi cha papa. Na kiti chake, kina taji yenye sehemu tatu. Nami niliiangalia hiyo taji moja kwa moja, nikisimama karibu kama vile mkono wangu ulivyo karibu na uso wangu, namna hiyo, na—na nikaona ile taji ya papa iliyopambwa kule Vatikani kwenyewe, mimi mwenyewe, nilisimama na kuiangalia, nipate kuwa na hakika ninajua ninalozungumzia. "Yeye ajiinuaye, nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, watu wote wanaomcha Mungu. Yeye ndiye mtakatifu kuliko wote hao; anaketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha tu nafsi yake kana Kwamba yeye ndiye Mungu," akisamehe dhambi duniani, na kadhalika, unajua. Kweli.

185 Paulo alisema, "Itabidi ule ukengeufu uje kwanza, yule mwana wa uharibifu afunuliwe."

Je! hamkumbuki ya kuwa wakati nilipokuwepo pamoja nanyi naliwaambieni hayo?

186 Loo, laiti ningalikuwa nimeketi pale, kumsikiliza Paulo akihubiri hayo. Mnaonaje? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Aha! jinsi ningetaka kumsikiliza yeye. Loo, jamani!

187 Sasa yeye atafanya jambo gani? "Sanamu ya mnyama." Wathesalonike wa Pili. Sasa sikilizeni. Sikilizeni kwa makini sasa, kwa makini hasa. Kanisa lilikuwa tayari linahisi kule kuja kwa papa. Ni kitu gani? Ule mwisho wa wakati huo wa kanisa, Paulo. Waliona upuuzi huu wa Wanikolai ulikuwa ukiinuka; walikuwa wanataka kufanya mtu mtakatifu, (kuwa kitu gani?) papa. Ulimwengu na matajiri walikuwa wamepenya kanisani, na kubadilisha utaratibu wa ibada. Paulo, akiwa na Roho Mtakatifu, alikuwa ameshika jambo hilo katika Roho. Nalo kanisa, pamoja na tabaka zake na wakubwa, waheshimiwa, na kadhalika, kwamba waliona kitu fulani kilikuwa kinakuja. Naye Roho Mtakatifu alikuwa akiwaonya juu ya siku za mwisho. Je! hamkumbuki jinsi Yesu alivyonena juu yake? Matendo ya Wanikolai, ambayo hatimaye yalifanyika fundisho, halafu yakawa madhehebu! Ndugu, hatuko katika giza sasa. Kumbukeni, mnaona. Tumefika.

188 Matendo ya Wanikolai, madhehebu yakaanza kuingia, waheshimiwa maarufu, na kwenye makanisa, na kadhalika, ndipo kukaundwa kanisa Katoliki. Na Paulo alisema hakuwezi kuweko na wakati wa mwisho, hapawezi kuwepo na wakati, mpaka kuwepo na ukengeufu kutoka kwenye Imani halisi ya kipentekoste. Imani ya kipentekoste itaondolewa, na waheshimiwa wataingia. Watakuwa na mtu atakayepachukua mahali pa Mungu, atakayeketi katika hekalu la Mungu, na ajiinue, nafsi yake juu ya watu wote wa namna hiyo. Na, hicho, mnaona ni kitu gani? Nikao "kuwashinda washiriki." Mnaona? "Yote yaitwayo Mungu; ataketi katika hekalu lake la Mungu, kama Mungu." Paulo alisema, "Kutakuweko na ukengeufu, kwanza, katika siku za mwisho." Basi tumewasili, kabisa sasa, na kuona huo ukengeufu, na kuona kanisa likikengeuka zaidi na zaidi kutoka Kwake, na kurudi nyuma moja kwa moja tena. Nasi tuko katika wakati wa mwisho. Vema.

189 Sasa, kama yale majuma sitini na tisa yalitimia kikamilifu, na Wayahudi wako katika nchi ya uenyeji wao sasa, na wakati wa kanisa la Mmataifa umefikia kwenye wakati wa mwisho kabisa, kufikia wakati wa Wanikolai . . . ama kufikia wakati wa Laodikia; je! kule Kuja kwa Bwana, mwisho wa mambo yote, mwisho wa wakati huu, na kule Kunyakuliwa kuko karibu jinsi gani? Mara atakapoanza juma hilo la sabini, ama ile miaka saba, Kanisa limeondoka.

190 Mnaweza kuona jambo hilo, marafiki? Inua mkono wako kama unaweza kuona jambo hilo. Mnaona? Sasa, hebu na tusiwe

watoto. Hebu tusicheze tena. Tuko katika wakati wa mwisho. Jambo fulani liko karibu kutukia. Tuko mwishoni. Tumewasili.

191 Haya majuma sitini na tisa yametimia kikamilifu; kule kuondoka kwa Wayahudi kulitimia kikamilifu; wakati wa kanisa ulitimia kikamilifu. Tuko katika wakati wa mwisho, wakati wa kanisa la Laodikia, mwisho wake. [Ndugu Branham anatumia ubao kuelezea—Mh.] Wale wajumbe nyota wote wamehubiri ujumbe wao. Umetangazwa. Tuko tu karibu na ukingoni. Wayahudi wamekuwa wakirudi kwa miaka arobaini. Wako kwenye nchi ya uenyeji wao.

Jambo linalofuata ni lipi? Kule kuja kwa lile Jiwe. Mambo ndiyo hayo. Ni wakati gani litatukia? Sijui. Lakini, ndugu, kwangu mimi, ninataka kuwa tayari. Ninataka kuandaa nguo zangu kabisa.

192 Sasa, tunaninii tu—tuna dakika chache tu, nami ningetaka sana kama mngalisikiliza kwa utulivu sasa kwa muda kidogo tu.

Mara Yeye atakapoanza lile juma la sabini, ama ile miaka saba, kanisa limeondoka. Sasa sikilizeni. Ninanukuu tena, kunukuu tena, msije mkasahau. Haya ndiyo Roho Mtakatifu aliyoweka kwenye kalamu yangu wakati nilipokuwa nikiandika. Tuko katika wakati wa Laodikia. Kristo anakataliwa na kanisa Lake mwenyewe. Yule mjumbe wa wakati huu, ule Ujumbe, umetolewa. Nao Israeli wako katika nchi yao. Mnaona mahali tulipo? Tuko mwishoni.

Sasa, tamshi moja ama mawili tu.

193 Yote haya sasa tunayoona, yatatusaidia, kwa neema Yake, tunapojitahidi kuiendea hii Mihuri Saba ya mwisho. Mnaona mahali ambapo tungaliyakosa? Kutoka Ufunuo 6:1 hadi Ufunuo 19:21, tungaliyakosa, maana, unaona, tungalikuwa tunajaribu kuyaingiza kwa nyuma, katika wakati huu wa Mataifa; ambapo, mnaona, yako kwenye wakati huu. [Ndugu Branham anatumia ubao kuelezea—Mh.] Mnaona?

Sasa, tumethibitisha jambo hilo kwa Neno la Mungu, na kwa historia, na kwa kila kitu, na kwa ishara za wakati, kwa siku, ya kwamba hakuna kitu kingine kilichosalia. Tuko mwisho wa Mataifa. Tuta—tutafanya nini juu ya jambo hilo? Ni nafsi yangu na nafsi yako; ni maisha yangu na maisha yako; ni maisha ya wapenzi wetu. Tumebembelezwa mno. Tumepata mambo mengi kwa urahisi sana. Afadhali tuanze kusonga mbele. Wakati umeenda mno kuliko unavyodhania, kumbukeni tu.

194 Sasa, tamshi la kushangaza, ukitaka kuliandika. Tafadhali sikilizeni kwa makini. Hili ndilo tamshi langu la mwisho, linalofuatia hilo; nina jambo dogo hapa mara tu baada ya hili, muhtasari mdogo ninaotaka kunena habari zake. Sasa ngojeni kwa muda kidogo tu na msikilize kwa makini, niwape jambo fulani ambalo linashangaza, kuambatana moja kwa moja na hili. Mnaona?

Hakuna hata upana wa ubapa wa kisu kati ya mwisho wa wakati huu na kule Kuja kwa Kristo. Kila kitu, hakuna kitu kingine kilichosalia. Je! Israeli yuko katika nchi ya uenyeji wake? Tunajua jambo hilo. [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Tuko katika wakati wa Laodikia? ["Amina."] Je! ujumbe wa wakati huu wa Pentekoste umetangazwa, kujaribu kuwatikisa watu warudi kwenye Baraka ya asili ya pentekoste? ["Amina."] Je! Kila mjumbe amepitia katika wakati, jambo lile lile hasa? ["Amina."] Mataifa yanapigana na mataifa? ["Amina."] Tauni? Kuna njaa nchini leo, Kanisa la kweli likisafiri mamia ya maili kwa gari wakitafuta kusikia Neno la Mungu? ["Amina."] "Si kwa ajili ya mkate peke yake, lakini kwa ajili ya kulisikia Neno la Mungu." Kumetokea njaa. ["Amina."] Hiyo ni kweli? ["Amina."] Mbona, tunaishi kabisa sasa katikati yake, papa hapa sasa. ["Amina"]. Mnaona mahali tulipo? ["Amina"] Tunangojea Jiwe lile.

195 Tamshi la kushangaza! Tangu wakati Mungu alipomtolea Ibrahimu ahadi... Msikose jambo hili. Tangu wakati Mungu alipomtolea Ibrahimu ahadi, Mwanzo 12:3, hadi wakati wa kule kukataliwa kwa Kristo katika 33 B.K.; na Wayahudi kulingana na Wagalatia 3:16 na 17, na kulingana na kitabu cha Usher, cha U-s-h-e-r, kitabu cha Usher cha ukoo wa Waebrania; nguvu za Mungu zilikuwa pamoja na Wayahudi kwa muda mwa miaka elfu moja mia tisa hamsini na nne kamili. Mungu alishughulika na Wayahudi kwa miaka elfu moja mia tisa na hamsini na nne, kulingana na ukoo wa Wayahudi, na kulingana na Wagalatia 3:16 na 17. Nina Maandiko mengi zaidi, lakini nitawapa hayo tu.

Halafu, baada ya kumkataa Kristo, Yeye aliwaendea Mataifa, apate kuwachukua watu kwa ajili ya Jina Lake. Mnataka Maandiko kwa ajili ya jambo hilo, mahali lilipo? Matendo 15:4.

196 Sasa, tukihesabu wakati, tunaona ya kwamba tuna miaka (sikilizeni) kumi na saba iliyosalia barabara, nasi tutakuwa tumepewa kipindi kile kile cha wakati, kama ambavyo Mungu ametushughulikia katika nguvu za Roho Mtakatifu, tangu mwaka wa 33 B.K. mpaka 1977. Kipindi kile kile sawa cha wakati, cha miaka elfu moja na mia tisa hamsini na minne, Mungu akitushughulikia sawa na alivyowashughulikia Wayahudi. Mnalionaje hilo!

197 Sasa, andika katika kitabu chako, Maandiko machache hapa ninayotaka kuwapa. Mambo ya Walawi 25, kuanzia aya ya 8. Mungu aliagiza yubile kila mwaka wa arobaini na tisa. Mwaka wa hamsini ulikuwa ni yubile. Tunajua jambo hilo. Tunafahamu jambo hilo. Tangu yubile ya kwanza, ya Mambo ya Walawi 25:8, katika mwaka wa 1977 itakuwa ni yubile ya sabini, ikifanya miaka elfu tatu mia nne na thelathini kamili. *Yubile*, maana yake, "Kwenda juu! Kule kuachiliwa!"

Loo, tunakungojea kule kuja kwa Siku ile ya furaha ya ule Utawala wa Miaka Elfu,
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja na kumnyakua kwenda naye Bibi-arusi Wake anayengoja;
Loo, ulimwengu unaugua, ukiililia siku hiyo ya kuwekwa huru kutamu,
Wakati Mwokozi wetu atakaporudi duniani tena.

198 Mlilipata jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina"—Mh.] Mungu ameshughulika nasi kwa muda ule ule kamili aliowashughulikia Wayahudi. Tangu wakati aliompa Ibrahimu ile ahadi, mpaka kule kukataliwa kwa Masihi katika 33 B.K., ilikuwa miaka elfu moja mia tisa na hamsini na nne. Na sasa tuna miaka kumi na saba iliyosalia. Tulikuwa na kama miaka elfu moja mia tisa na thelathini na kitu. Tuna miaka kumi na saba iliyosalia, kufikia '77, itakuwa ni yubile ya sabini tangu mwanzo wa yubile. Na itakuwa ni nini? Loo, ndugu! Angalia kwa makini sasa. Usikose jambo hili. Itakuwa ni yubile ya kupaa juu kwa Bibi-Arusi wa Mataifa, na kurudi kwa Kristo kwa Wayahudi, watakapotoka utumwani. Amina! Hamwoni? Kutoka ulimwenguni kote, wamekusanyika kule kwa ajili ya siku hiyo. Loo, jamani! Mnaona mahali tulipo? Hatujui ni wakati gani jambo hilo huenda litaweza kutukia. Tuko katika wakati wa mwisho.

199 Sasa sikilizeni. Kwenu ninyi watu wa zamani hapa ka—kanisani, ambao mmekuwa hapa kwa muda mrefu, ninataka mwangalie jambo fulani. Sikujua jambo hili mpaka jana; nililichukua kutoka kwa mwanahistoria, Paul Boyd, na halafu. . .nami nimelifuatilia katika Maandiko, nikazichukua tarehe hizi nyiingine hapa, na kadhalika, na kulipata, na kulifuatilia, nikalifuatilia kila mahali.

200 Sasa, katika mwaka wa 1933, tulipokuwa tukiabudia hapa katika hekalu la Masonic, ambapo kanisa la Kristo linasimama leo. Katika asubuhi moja ya Aprili, kabla sijaondoka nyumbani . . .

Nilikuwa nikiweka wakfu gari langu. Nilikuwa na gari la muundo wa '33, nami nilikuwa nikiliweka wakfu kwa utumishi wa Bwana. Na katika ono, niliona wakati wa mwisho. Sasa angalia jinsi jambo hili lilivyo la kushangaza, kule nyuma wakati nilipokuwa kijana tu. Nanyi mnaweza kuwazia jinsi gari la muundo wa 1933 lilivyokuwa, sasa, jinsi lilivyokuwa.

Nami nilienda kule kwenye hekalu la Masonic, ambako . . . Baadhi yenu ninyi watu wa zamani hapa mnakumbuka. Limeandikwa katika gazeti la zamani, huko nyumbani. Limechapishwa tayari na kusambazwa ulimwenguni kote. Mnaona? Hiyo ilikuwa katika mwaka wa 1933. Nami nilitabiri ya

kwamba kuna msiba mkubwa utakaoipata nchi hii ya Marekani kabla ama ifikapo mwaka wa 1977. Ni wangapi wanakumbuka nikisema jambo hilo? [Watu wa zamani wanasema, "Amina."] Angalieni hiyo mikono. Hakika.

201 Sasa angalia. Nilitabiri mambo saba bado yanataka kutukia...kabla ya huu ukomo mkuu ama jambo kubwa kutukia hapa Marekani, jambo kubwa la kutisha. Nilisema . . .

Sasa kumbukeni, hii ni kabla havijaanza. Nilisema tutaingia katika Vita vya Pili vya Dunia. Ni wangapi wanakumbuka wakinisikia nikisema jambo hilo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Vita vya Pili Vya Dunia! Nikasema, "Rais tuliye naye sasa ni . . . " Nilinakiri haya kutoka kwenye maandiko ya zamani, hata hivyo, jambo lile la zamani jana, ya kwamba, "Rais tuliye naye sasa," ambaye alikuwa... Ni wangapi wanaokumbuka alikuwa ni nani? [Ndugu fulani anasema, "Franklin Roosevelt."] Franklin D. Roosevelt. Nilisema, "Rais tuliye naye sasa atapigiwa kura hata kwenye kipindi cha nne," alikuwa katika kipindi chake cha kwanza wakati huo, "ataendelea hata kwenye kipindi cha nne, nasi tutaingizwa katika Vita vya Pili vya Dunia."

202 Nikasema, "Yule dikteta ambaye sasa anainuka huko Italia, ambaye ni Mussolini, yeye ataingia madarakani. Kisha ataenda Ethiopia, na Ethiopia itashindwa kwa urahisi." Kuna watu wanaoketi hapa sasa wanaojua, ya kwamba kuna kundi la watu waliokuja na kusimama, nilipokuwa nikifanya mkutano wangu katika Ukumbi wa Redman chini kule usiku huo, iliponibidi nishuke kwenda kule na kuhubiri jambo hilo, Ukumbi wa Redman, nao walikuwa wanataka kunitupa nje ya ukumbi huo kwa kusema jambo kama hilo. [Dada Wilson anasema, "Amina. Hiyo ni kweli."—Mh.] Naam. Naam. Bibi Wilson, ninajua una-. . . ["Hiyo ni kweli."] Hiyo ni kweli. Niliposema jambo hilo . . . Lakini je! alifanya jambo hilo? "Lakini," nilisema, "mwisho wake utakuwa wa aibu," naye alifanya jambo hilo. Yeye na mwanamke aliyeambatana naye, walipinduliwa juu chini na wakaning'inizwa kwenye kamba barabarani, miguu yao juu, nguo zao zikining'inia chini. Vema, jambo hilo lilitukia.

203 Kisha nikasema, "Wanawake wameruhusiwa kupiga kura. Jambo ambalo ni aibu kabisa kwa taifa. Na, katika kupiga kura, siku moja watamchagua mtu asiyefaa." Nao walifanya jambo hilo katika uchaguzi huu wa mwisho. Jamani, jamani! Nne...(Nilisema, "Sayansi itapiga hatua kubwa sana hivi kwamba . . . ") La, hapa, hilo ni la tatu. Samahani.

204 Hili hapa linalofuata, pale, la nne. Nilisema, "Vita vyetu vitakuwa dhidi ya Ujerumani, nao watajenga mahali pakubwa sana pa saruji na kujifanyia ngome humo, nao Wamarekani watapigwa vita vya kutisha." Mwenyezi Mungu anajua hilo, Yeye ambaye ninasimama mbele yake sasa, niliwaona hao

Wanazi huru wakiwapiga mateke Wamarekani hivyo, na kadhalika, kwenye huo ukuta. [Mtu fulani katika kusanyiko anasema, "Amina."—Mh.] Na kuna vijana wengi wanaosimama hapa sasa waliokuwa kwenye hiyo Ngome ya Siegfried, wanaojua ilivyokuwa. ["Amina. Naam, bwana. Amina."] Na kumbukeni, hiyo ilikuwa miaka kumi na moja kabla hiyo Ngome ya Siegfried kujengwa. Je! Mungu ni wa kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Yeye angali anatabiri mambo yatakayotukia? ["Amina."] Angalia. Hilo, hilo lilikuwa la nne.

205 Sasa jambo la tano. "Sayansi itapiga hatua kubwa sana hivi kwamba watafikia kuunda gari ambalo halitaongozwa kwa usukani. Na magari yataendelea kuundwa mfano wa yai, mpaka ukomo, ule mwisho. Niliona familia ya Kimarekani ikishuka kwenda barabarani, katika barabara pana, ikiendesha gari huku wameelekeza migongo yao mahali palipopaswa kuwa na usukani, ilionekana kana kwamba walikuwa wanacheza kamari ama karata." Nasi tunalo. Liko kwenye televisheni. *Popular Science, Mechanics*, hasa, yote yanalo. Tunalo gari hilo hilo. Linaongozewa na rimoti, kwa—kwa rada. Hata hawatakuwa na haja na usukani wo wote ndani yake. Ni kuweka tu bamba lako namna hii, kama vile unavyopiga simu, na gari lako linakubeba moja kwa moja; haliwezi kupata ajali, wala cho chote kile, hakuna magari mengine. Sumaku inayazuia hayo mengine yasikukaribie. Mnaona? Wanalo. Loo, jamani! Wazia jambo hilo. Ilitabiriwa miaka thelathini kabla halijatendeka!

206 Sasa, hilo linatuleta basi kwenye ule uchaguzi wa Rais Kennedy.

Na gari hili linalojitokeza ju—jukwaani, linaleta mambo matano (kutoka katika yale saba) ambayo yametukia vile vile.

207 Sasa, nilibashiri, na nimesema, "Nilimwona mwanamke mkubwa amesimama, anayependeza, amevikwa mavazi ya zambarau safi kama ya kifalme. Nami nina mabano yenye maneno machache hapa, "(Yeye alikuwa mtawala mkuu Marekani; labda ni kanisa Katoliki.)" Mwanamke, mwanamke fulani; sijui kama itakuwa ni kanisa Katoliki. Sijui. Siwezi kusema. Jambo pekee nililoona, nilimwona mwanamke huyo, basi.

208 Lakini hili ni taifa la mwanamke. Taifa hili ni namba kumi na tatu, katika unabii. Lina milia kumi na mitatu, nyota kumi na tatu. Lilianza na koloni kumi na tatu. Kumi na tatu, kumi na tatu, kila kitu ni kumi na tatu. Hata, linaonekana katika Ufunuo sura ya 13. Hili ni kumi na tatu. Na ni taifa la mwanamke.

209 Mahakama za talaka Marekani hutoa talaka nyingi sana, kutoka kwa wanawake wetu, kuliko mataifa mengine yote. Uadilifu katika nchi yetu umeshuka sana, na talaka, kuliko ilivyo katika Ufaransa ama Italia, mahali ambako umalaya uko mitaani. Kwa hiyo, lakini wao ni malaya; wetu ni wanawake

walioolewa wakikazana kuishi na wanaume wengi, na wanaume wengi waliooa wakikazana kuishi na wanawake wengine.

210 Katika mataifa ambako wanaoa wanawake wengi, ni nafuu mara elfu. Na, hata hivyo, kuoa wanawake wengi ni makosa, tunajua hivyo. Lakini, inaonyesha tu jinsi tulivyo duni.

211 Nina mkato pale kutoka kwenye gazeti, ambapo inaonyesha ya kwamba wakati vijana wetu wa Kimarekani walipoenda nchi za ng'ambo, katika vita hivi vilivyopita, ya kwamba zaidi ya ninii, ninaamini, ilikuwa kama asilimia sabini . . . Mbona, sasa, ngoja kidogo, ninaamini ilikuwa watatu kati ya wanne walioenda katika nchi za ng'ambo, waliotalikiwa na wake zao kabla hawajarudi. Na ni kichwa kikubwa mno cha maneno kinachosema, "Kumetokea nini kwa uadilifu wa watu wetu wa Mrekani?" Mnakumbuka mliliona hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninyi nyote, nadhani. "Kumetokea nini kwa uadilifu wa wanawake wetu wa Marekani?" Viwandani, wakifanya kazi kule na wanaume wengine. Ni taifa la wanawake. Atakuwa na nini? Mungu mwanamke, ama mungu wa kike.

212 Sasa, basi, baada ya jambo hilo, niligeuka na kuangalia. Nami nikaona hii Marekani ikiungua kama mwenge, miamba ilikuwa imelipuliwa. Na ilikuwa ikiungua kama lu—lundo la moto kwa magogo, ama kitu fulani kilichoiunguza tu. Nami nikaangalia umbali nilioweza kuona, nayo ilikuwa imelipuliwa. Ndipo hilo ono likaniacha. Matano kati ya hayo matatu yametukia . . . ama matano kati ya hayo saba, hasa, yametukia.

213 Na hapa anakuja na kuonyesha. Halafu nilibashiri. Sikusema kamwe ya kwamba Bwana aliniambia jambo hilo, lakini, nikiwa nimesimama asubuhi hiyo kanisani, nilisema, "Vile maendeleo . . . " Nilirudi katika mwisho mmoja wa ukuta wao, na kukimbia mpaka upande ule mwingine wa ukuta. Nikasema, "Vile maendeleo yanavyokwenda, nitabashiri ya kwamba wakati . . . Sijui ni kwa nini ninasema jambo hili. Lakini ninatabiri ya kwamba hayo yote yatatukia kati ya sasa hivi, 1933, na 1977."

Na bila kujua jambo hilo, Mungu anaujua moyo wangu, sikujua jambo hilo mpaka jana, ya kwamba 1977 ni yubile, na ni kipindi kile kile cha wakati kimekwisha ambacho Yeye aliwapa Israeli, na kila kitu mwishoni. Kwa hiyo sisi tuko . . . Na tumefikia hapa mwishoni mwa wakati, katika kule kuja kwa lile juma la sabini. Hatujui ni wakati gani kanisa litakapoondoka. Loo, jamani! Tufanyeje, enyi marafiki? Tuko wapi?

214 Mnaona tulivyo sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnafahamu lile juma la sabini la Danieli sasa? ["Amina."]

Mnaona, sasa, tutakapoenda katika Mihuri hii na kadhalika, kuivunja Mihuri hii. Wa kwanza unatokea, mpanda farasi mweupe, naye ana uta mkononi mwake. Angalia jamaa huyo

ni nani. Angalia huyu mpanda farasi wa kijivu akimfuata. Unaona? Angalia yeye ni nani, na uangalie jinsi wanavyoingia. Angalia Wale mia na arobaini na nne elfu wakiingia. Angalia huyo mwanamwali aliyelala atakapokuja. Kisha angalia mambo haya yote yakitukia, kule kumwagwa kwa vile Vitasa, zile Ole, wale roho watatu wachafu kama vyura. Angalia vitu hivyo jinsi vinavyoingiana na hayo mapigo, inalingana kabisa na wakati vitakapomwagwa. Kila wakati Mhuri ulipofunguliwa, pigo linamwagwa, na maangamizi yanatokea. Kisha angalia yanayotukia sasa hivi hapa kwenye wakati wa mwisho.

215 Na, loo, angalia hawa manabii watatu . . . ama hawa manabii wawili, wanainuka hapa. Na katikati ya hilo juma likiendelea, wanakatiliwa mbali namna hiyo, kisha vinaanza vile Vita vya Har-Magedoni. Ndipo Mungu anaanza kuzungumza, Yeye Mwenyewe, kisha anasimama na kuanza kupigana. Hao manabii wanaipiga dunia. Wanahubiri Jina la Yesu Kristo. Wanabatiza namna ile ile. Wanafanya jambo lile lile ambalo wale wapentekoste wa kwanza, mababa walivyofanya, na wengi wanawafuata. Lakini hao walioungana, madhehebu hayo, yaliendelea moja kwa moja, na hata nguvu za manabii hao hazikukivunja kitu hicho. Na hatimaye wakasema, "Tutaufanya wote shirika moja." Naye anaingiza (ni kitu gani?) lile chukizo, Urumi, kueneza jambo hilo lote, linalosababisha ukiwa. "Chukizo la uharibifu," linachukua kila kitu, "ule uchafu."

216 Kumbukeni, yule mama kahaba wa siku nyingi aliyeketi juu ya yule mnyama, aliyevikwa mavazi mekundu namna hiyo, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. Mnakumbuka jambo hilo? "Naye alikuwa na kikombe mkononi mwake, cha uchafu wa machukizo yake." Hilo lilikuwa ni fundisho lake alilowapelekea watu. Basi tumewasili, ndugu zangu. Tuko katika wakati wa mwisho.

217 Enyi watoto wadogo, hatujui kamwe, huenda tusiishi kupata kurudi tena usiku wa leo. Huenda tusiishi tukaonana tena. Sijui. Lakini, mwisho umekaribia sana, mwisho upo karibu sana. Haya hapa Maandiko. Hilo hapo thibitisho kamilifu kabisa la Kimaandiko.

218 Sasa, kama kuna jambo fulani hukulielewa, niandikie muhtasari mdogo juu ya jambo hilo nijue. Mnaona? Sema jambo fulani. Baadhi yenu ninyi ndugu huko nje kwenye kanda, katika sehemu hizo nyingine, kama kuna jambo fulani ninaloweza kuwasaidia, hebu nijue. Huenda usikubaliane nami, nami huenda nisikubaliane na shirika lako; si wewe, lakini utaratibu wa shirika lako. Mimi sitofautiani na Wakatoliki. Sisemi ya kwamba siwapendi Wakatoliki, kwamba siwapendi watu wa madhehebu. Sivyo hivyo. Ninawapenda watu wote, lakini sikubaliani na ule utaratibu unaokufunga. Jambo ndilo hilo, utaratibu wake. Jambo ndilo hilo.

219 Mimi sikuwa ninapinga Ujerumani; ilikuwa ni Unazi. Sikuwa ninawapinga Waitaliani; ilikuwa ni kinyume na—na ule Ufashisti. Pia kumbukeni, nilibashiri jambo lingine wakati ule, ubashiri tu, na wengi wenu ninyi watu wa zamani mnaukumbuka. Nilisema, "Kuna itikadi tatu kuu zinazojaribu kuutawala ulimwengu leo: Ufashisti, Unazi, na Ukomunisti." Na nilisema nini? "Zote zitaishia katika Ukomunisti."

220 Ndipo niliwafanya ninyi nyote kurudia hilo, "Angalia Urusi." Mnakumbuka hilo? "Usiondoe macho yako Urusi. Yote itaishia katika Ukomunisti."

Halafu zote zitaishia, hatimaye, katika Ukatoliki. Kumbukeni, zote zitaishia katika Ukatoliki katika wakati wa mwisho. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kwenye vita vya Har-Magedoni, moja kwa moja *hapa*, wakati atakapokuja Kristo, Mwenyewe.

221 Lakini hawa manabii watatu. . .Hii miaka mitatu na nusu, hasa, hiyo ni Ufunuo 11:3, mmelisoma mara nyingi, "Nami nitawapa nguvu mashahidi Wangu wawili, nao watatabiri siku elfu na mia mbili na sitini." Ni miaka mingapi, hizo siku elfu na mia mbili na sitini? Miaka mitatu na nusu. "Kisha watauawa katika njia za mji," katikati kabisa ya lile juma la sabini.

Kwa hiyo, mnaona yalipo yale majuma sabini ya Daniel? Mnaona mahali tunapoishi? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Tuko mwisho, rafiki zangu wapendwa. Tuko mwisho. Zile siku . . .

Mataifa yanavunjika, Isreli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii; (Tumewasili.)
Siku za Mataifa zimehesabiwa, (*hapa*) zimekumbwa na hofu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

Hebu tuuimbe:

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

Loo, jamani! hilo si ni zuri sana?

Mataifa yanavunjika, Isreli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

Sasa pamoja.

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni Roho, taa zenu nimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu unakaribia!

Hebu niwaimbieni ubeti mfupi.

Manabii wa uongo wnadanganya, Kweli ya Mungu wanaikana,
Ya kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu wetu;

Wao wanamfanya Yeye Nafsi fulani ya tatu. Mnajua jambo hilo. Lakini, Sivyo alivyo. Yeye ni Mungu wetu.

Lakini tutatembea walipotembea mitume.

Kwa kuwa siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

222 Je! hamna furaha? Rudi kwenye Ujumbe, ndugu! Rudini kwenye ile ya asili! Rudini pentekoste! Rudini kwenye baraka halisi! Rudini kwenye Jina la Yesu Kristo! Rudini kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu! Rudini kwenye ishara na maajabu! Rudini pentekoste! Tupilieni mbali madhehebu! Rudini kwa Roho Mtakatifu! Yeye ndiye Mwalimu wetu.

Kwa kuwa siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!

223 Huo si ni mzuri sana? Nabii alisema nini? “Utakuja wakati ambapo itakuwa, huwezi kusema ni usiku au mchana.” Angalia jinsi ilivyokuwa. Unaona? Loo, ni mbaya sana, katika nyakati za kanisa!

Lakini i—itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Kijia cha Utukufuni hakika mtakipata;
Katika njia ya maji ndiko kwenye Nuru leo,
Ukizikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani;
Hizi Nuru za jioni zimekuja,
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

Itakuwa Nuru (Nyote pamoja!) wakati wa jioni,
Kijia cha Utukufuni hakika mtakipata;
Katika njia ya maji ndiko kwenye Nuru leo,
Ukizikwa katika Jina la thamani la Yesu.

Vijana na wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani.
Kwa kuwa Nuru za jioni zimekuja,
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.
(Si watatu; lakini Mmoja!)

224 Rudini kwenye Ujumbe! Rudini huko mwanzo! Rudini kwa yale aliyofundisha Paulo! Rudini kwenye ubatizo aliobatizia! Yeye aliwaona watu wamebatizwa vingine; akawaambia waje wabatizwe tena. Akasema, "Kama Malaika akija kutoka Mbinguni, angehubiri jambo lingine lo lote, na alaaniwe." Kwa hiyo, ni kurudi kwenye Ujumbe tena, ewe rafiki! Ni wakati wa jioni.

225 Loo, ninampenda sana! Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wanaoliona juma la sabini la Dnieli sasa, na kuona kwamba lile juma la sabini ni kitu gani? Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? Semeni, "Amina." ["Amina!"] Amina! Mungu asifiwe!

226 Sasa, jambo linalofuata ni lipi? Ile Mihuri Saba sasa. Tunaiendea moja kwa moja, Bwana takapoturuhusu. Kwamba itakuwa ni wakati gani huo, sijui. Ni wakati wo wote ule atakapozileta, ndipo tutaingia moja kwa moja katika hilo. Ndipo tutakuwa na mkutano mrefu, mrefu sana, kwa maana itachukua kutoka mlango wa 6 hadi wa 19, kulipitia, na vile ninavyoenda pole pole nalo.

227 Sasa, sitaki mtu ye yote aondoke akielewa vibaya jambo hili. Kanda ingali inachezwa. Sitaki mtu ye yote afahamu vibaya. Msielewe vibaya sasa, na kusema, "Ndugu Branham alisema Yesu atakuja katika mwaka wa 1977." Sikusema jambo kama hilo kamwe. Yesu anaweza kuja leo. Lakini nimebashiri ya kwamba kati ya mwaka wa '33 na '77 jambo fulani litatukia, ya kwamba mambo haya ambayo nimeona yakija kutimia, katika ono, yatatimia. Na matano ya hayo yametukia tayari. Nami ninaamini, tukiwa na vile vitu vya atomiki tulivyo navyo sasa. . .

228 Na mliona yale Rais wetu alivyosema hivi karibuni? Anataka vita vingine. Yeye anataka kuifanya Berlin i—ione cha mtema kuni, ndivyo alisema. Alitaka waone cha mtema kuni. Na jirani yetu Cuba hapa karibu nasi je? Mbona asiifanye ione cha mtema kuni? Vipi kuhusu hiyo? Loo, ni upuuzi mtupu! Mnaona?

229 Loo, ndugu, tuko tu mwishoni. Wao wataninii. . .Litatukia tu jinsi Mungu alivyosema litatukia, kwa hiyo ya nini—ya nini kufanya jambo lo lote mbali na kusoma yale Yeye aliyosema, na kuwa sawa na kujiandaa kwa ajili ya jambo hilo. Ndipo acha ije, basi. Tunaingojea.

Tunakungojea kuja kwa ile Siku ya furaha ya ule Utawala wa Miaka Elfu,
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja kumchukua Bibi-arusi Wake anayengoja;
Loo, dunia inaugua, ikililia ile siku ya kuwekwa huru kutamu,
Wakati Bwana wetu atakapokuja duniani tena.

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Naam, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Loo, Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa na mjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

Ni wangapi walio tayari? Inua mkono wako. Loo, jamani!

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,

Hebu na tusimame tu na tpeane mikono.

Bwana wetu anarudi duniani tena,
Loo, Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa na mjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Bwana wetu anarudi duniani tena,
Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa na mjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

Kurudi kwa Yesu kutakuwa ndiko jibu la huzuni na kilio kwa dunia,
Kwa maana maarifa ya Bwana yataijaza dunia, bahari na mbingu;
Mungu ataondoa magonjwa yote na majonzi ya mateso yatakauka,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Naam, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Loo, Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa na mjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

230 Loo, jamani! Hivi hamjisikii vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina! Haleluya!"—Mh.] Wazieni, enyi marafiki, hii ni ya kipentekoste, ibada! Hii ni pentekoste. Hebu na tupige makofi na kuuimba. Wapentekoste, kila mtu, sasa jiachilie, ondoa hiyo desturi ya kale ya Kimethodisti ndani yako. Hima, na tuuimbe!

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Naam, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa namjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

Loo, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Naam, Bwana wetu anarudi duniani tena,
Loo, Shetani atafungwa miaka elfu, hatutakuwa na mjaribu wakati huo,
Baada ya Yesu kurudi duniani tena.

Mnampenda? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Vema. Ninampenda. *Ninampenda*, Dada Gibbs. Loo, hebu na tumwinulie tu mikono yetu.

Ninampenda, ninampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua woko-. . .(Wapi? Papa hapa Kalvari.)
Mtini Kalvari.

Ninampenda, (Utukufu!) ninampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Maagizo Ya Gabrieli Kwa Danieli
(*Gabriel's Instructions To Daniel*)
30 Julai, 1961, Jumapili asubuhi

Sababu Sita Za Kusudi La Gabrieli Kumzuru Danieli
(*The Sixfold Purpose Of Gabriel's Visit To Daniel*)
30 Julai, 1961, Jumapili jioni

Lile Juma La Sabini La Danieli
(*The Seventieth Week Of Daniel*)
6 Agosti, 1961, Jumapili asubuhi

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kwenye Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamili zaidi, kitabu hiki cha Neno Lililonenwa cha *Yale Majuma Sabini Ya Danieli* kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Uilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org